BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,001,641,108/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 4

**NESI** adaiwa kukamatwa na dawa za kulevya


HOTUBA

Nipashe 11

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII, MHE. BALOZI DKT. PINDI HAZARA CHANA (Mb), WAKATI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/23

MHE. BALOZI DKT. PINDI HAZARA CHANA (Mb) WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII

DKT. FRANCIS KASABUBU MICHAEL KATIBU MKUU WA MALIASILI NA UTALII

MHE. MARY FRANCIS MASANJA (Mb) NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII

BW. JUMA SELEMANI MKOMI NAIBU KATIBU MKUU WA MALIASILI NA UTALII

# Nipashe

Jumamosi Juni 4, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580966

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11



Aliyekuwa Askofu wa (KKKT), Dayosisi ya Konde, Dk. Edward Mwaikali, akitoka mahakamani jana, baada ya kesi kumalizika.

# Kesi mgogoro KKKT yatupwa

**ASKOFU** mpya Dayosisi ya Konde kusimikwa rasmi kesho... *Endelea Ukurasa 2*

# KISHINDO CHA UTALII

UKURASA 4

1. MATAJIRI BULGARIA KUJENGA HOTELI NCHINI
2. MAWAKALA WA UTALII WAMIMINIKA
3. FARU, TEMBO WAONGEZEKA HIFADHINI
4. NYUMBA ZAIDI WANAOHAMA NGORONGORO
5. TEKNOLOJIA YA KISASA KUFUATILIA WANYAMA



Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023, bungeni Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Tume yasema watuhumiwa wanateswa na kuuawa polisi

UKURASA 2

**MICHEZO** TAIFA STARS YAANZA KUISAKA AFCON LEO UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Tume yasema watuhumiwa wanateswa, kuuawa polisi

**Na Beatrice Shayo**

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imesema katika uchunguzi ilioufanya, imebaini kupigwa na kuteswa kwa watuhumiwa wakati wa ukamataji ama wakati wa upelelezi kwa madhumuni ya Jeshi la Polisi kupata taarifa zinazohusu matukio ya uhalifu.

Kutokana na vitendo hivyo, tume hiyo imebaini baadhi ya watuhumiwa kupata madhara ya mwili na wakati mwingine kupoteza maisha.

THBUB pia imebaini askari polisi wanaopatikana na hatia, kupewa adhabu isiyowiana na kosa husika walilolifanya.

Jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa THBUB, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu, alibainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusiana na tathmini waliyoifanya na utendaji kazi wa jeshi hilo.

Jaji Mwaimu alisema kwa mujibu wa sheria, wamepewa mamlaka magereza au sehemu wanapozuiliwa watu, kukagua uzingatiaji wa haki za binadamu katika sehemu hizo.

Alisema jukumu la msingi la Jeshi la Polisi ni kulinda usalama wa raia na mali zao na majukumu mengine yaliyoainishwa katika Sheria za Jeshi la Polisi ikiwamo kukamata, kufanya upekuzi, kuwaweka watuhumiwa mahabusu, kufanya upelelezi kuhusiana na matukio ya uhalifu na kufanya mahojiano na watuhumiwa.

Jaji Mwaimu alisema tathmini ya ujumla ya THBUB inaonyesha kuwa jeshi hilo linafanya kazi zake vizuri na ndiyo maana kwa sasa kuna amani na utulivu nchini na uhalifu umepungua.

"Tathmini ya ujumla kwa nyakati tofauti kumekuwa na malalamiko kutoka kwa watuhumiwa na wananchi na wakati mwingine kupitia vyombo vya habari, kulalamikia Jeshi la Polisi kuhusu matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora," alisema.

Kiongozi huyo alibainisha kuwa mwaka 2020 hadi 2022 THBUB imekuwa ikifuatilia mwenendo na utendaji kazi wa Jeshi la Polisi kwa kufanya uchunguzi (matukio 10) kuhusu tuhuma dhidi ya jeshi hilo na kutembelea vituo vya polisi katika baadhi ya mikoa nchini.

Alisema THBUB imekuwa ikiwatembelea mahabusu waliozuiliwa katika magereza ambako ilipata taarifa za malalamiko ya mahabusu kuhusu kuvunjiwa haki zao walipokuwa katika mahabusu ya polisi.

Jaji Mwaimu alisema uchunguzi wao wameufanya katika wilaya za Kinondoni, Ubungo na Ilala katika Mkoa wa Dar es Salaam, Mwanga mkoani Kilimanjaro, Kilosa na Mvumero mkoani Morogoro, Tabora mjini mkoani Tabora, Mafinga (Iringa), Handeni (Tanga), Masasi (Mtwara) na Mkoa wa Mjini Magharibi (Zanzibar).

Alisema katika kipindi hicho THBUB ilitembelea baadhi ya vituo vya polisi kwa lengo la kukagua uzingatiaji wa haki za binadamu katika vituo hivyo.

"Vituo vilivyotembelewa ni kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Dodoma, Mwanza, Ruvuma, Lindi na Mtwara. Mingine ni Mjini Magharibi, Kaskazini Unguja, Kusini Unguja, Kaskazini Pemba na Kusini Pemba," alisema.

Alibainisha kuwa katika uchunguzi huo wamebaini kupigwa na kuteswa kwa watuhumiwa wakati wa ukamataji au wakati wa upelelezi ukiendelea kwa madhumuni ya jeshi hilo kupata taarifa zinazohusu matukio ya uhalifu.

Alisema pia wamebaini kuwapo tuhuma za rushwa dhidi ya askari, baadhi ya askari polisi kutoa taarifa zisizo sahihi kuhusu vitendo wanavyolalamikiwa na wananchi na askari polisi wanaopatikana na hatia kupewa adhabu isiyowiana na kosa husika.

Alisema askari anapofanya makosa ya kujeruhi mtuhumiwa ama kusababisha kifo, anatakiwa kuwajibishwa kwa kosa la jinai badala ya kupewa adhabu ya nidhamu.

Alisema tume pia imebaini baadhi ya watuhumiwa kuwekwa mahabusu za polisi kwa muda mrefu bila ya kupelekwa mahakamani au kupewa dhamana.

Alisema katika kutekeleza wajibu wake wa kuishauri serikali baada ya kufanya uchunguzi, THBUB imependekeza kwa lengo la kuleta ufanisi na kuepuka vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, Jeshi la Polisi lihakikishe utendaji wake wa kazi unazingatia sheria, kanuni na miongozo ya utekelezaji wa majukumu yake.

Alisema makosa yanayofanywa na askari polisi yenye mwelekeo wa kijinai, yachunguzwe kwanza na taasisi nyingine huru za umma au vyombo ambavyo vitaweza kuundwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema kwa ajili ya kuongeza ufanisi, Jeshi la Polisi litekeleze mapendekezo yanayotolewa na tume hiyo huku akiitaka serikali kuliimarisha jeshi hilo kwa kulipatia vitendea kazi, kuendelea kuwajengea makazi bora, kuongeza idadi ya askari na kuimarisha miundombinu.

Jaji Mwaimu alisema wananchi waendelee kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo ili kusaidia kuzuia na kupambana na vitendo vya uhalifu nchini.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, akisalimiana na Mfalme wa Sweden, Mtukufu Carl XVI Gustav, alipomtembelea na kufanya mazungumzo katika nyumba ya kifalme Stockholm, nchini Sweden, baada ya ufunguzi wa Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Stockholm +50 unaoendelea nchini humo. **PICHA: OMR**

# Kesi mgogoro wa KKKT yatupwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

YAMEKWISHA. Ndivyo inavyoonekana baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya kutupa kesi iliyofunguliwa na aliyekuwa Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Konde, Dk. Edward Mwaikali.

Dk. Mwaikali na wafuasi wake walifungua kesi kupinga kuondolewa kwake madarakani kutokana na mgogoro ulioiandama Dayosisi hiyo kwa takriban miaka miwili baada ya kuhamisha makao makuu ya dayosisi kutoka Tukuyu mjini kwenda Usharika wa Ruanda, jijini Mbeya.

Kutokana na kutupwa kwa kesi hiyo, hofu ya zuio la kusimikwa kwa Askofu Mteule Mchungaji Geoffrey Mwakihaba na kuingizwa kazini msaidizi wake, Dk. Meshack Njinga, imemalizika. Kwa mantiki hiyo, Mchungaji Mwakihaba atasimikwa rasmi kesho na kuchukua uongozi wa dayosisi hiyo.

Mwaikali aliondolewa katika Mkutano Mkuu Maalum wa Dayosisi uliofanyika Machi, mwaka huu, Uyole jijini Mbeya, baada ya Kamati ya KKKT Makao Makuu iliyoundwa kusuluhisha mgogoro huo, kuagiza hatima ya mgogoro huo iamuliwe na Mkutano Mkuu wa Dayosisi ambacho ndicho chombo cha juu kabisa katika uamuzi wa masuala ya dayosisi.

Kutokana na kuondolewa huko, Mwaikali alifungua kesi mbili Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya kupinga hatua hiyo kwa madai kuwa mkutano huo ulikuwa batili. Katika kesi hiyo, pia alimshtaki Mkuu wa KKKT, Askofu Dk. Fredrick Shoo.

Akitoa uamuzi wa kesi hiyo jana, Jaji James Karayemaha alisema anatupilia mbali kesi zote mbili ambazo ni Na. 3 na 14 za mwaka 2022 na kuruhusu sherehe za kumweka wakfu askofu mpya ziendelee kama ilivyopangwa.

Jaji Karayemaha alisema mleta maombi, Djk. Mwaikali, hakufuata utaratibu wa kusuluhisha mgogoro huo kwa mujibu wa Katiba ya KKKT.

Alisema alichotakiwa kukifanya ni kushughulikia mgogoro huo kwa kufuata katiba ya kanisa kupitia mkutano mkuu badala ya kuifuata katiba ya Dayosisi pekee kabla ya kupeleka shauri hilo mahakamani.

Jaji Karayemaha alisema baada ya kupitia nyaraka mbalimbali na rejea kuhusu kesi hiyo, alisema suala hilo ni la kidini, hivyo mahakama haina mamlaka ya kutoa uamuzi badala yake wahusika katika mgogoro huo warudi katika meza ya mazungumzo ili kuumaliza.

Akisoma rejea za ushuluhishi wa migogoro ya aina hiyo iliyofanywa na majaji wengine, Jaji Kareyemaha alisema kwa sababu mgogoro huo unahusu dini, mahakama haina mamlaka ya kutolea uamuzi, hivyo hakuna haja ya kuendelea na shauri hilo mahakamani.

Alishauri mgogoro huo ushuluhishwe nje ya mahakama na kwamba endapo upande wa mleta maombi haujaridhika na uamuzi wa mahakama, una haki ya kukata rufani.

Baada ya kutolewa kwa uamuzi hayo, nje ya viunga vya mahakama, Wakili wa Dk. Mwaikali, William Mashoke alisema wanajiandaa kukata rufani kuhakikisha haki inapatikana.

Wakili wa wajibu maombi, Dk. Daniel Pallangyo, aliishukuru mahakama kwa kutenda haki. Alisema licha ya wateja wake kushinda shauri hilo, aliwaomba waumini na viongozi wa kanisa hilo kuendeleza amani na mshikamano kama maagizo ya Mwenyezi Mungu yanavyoagiza na kumaliza tofauti zao.

**CHANZO CHA MGOGORO**

Mgogoro wa KKKT Dayosisi ya Konde uliibuka baada ya Dk. Mwaikali kuhamisha makao makuu kutoka Tukuyu mjini kwenda Ruanda kwa kile alichadai kwamba jambo hilo lilipata baraka za Halmashauri Kuu ya Dayosisi.

Hata hivyo, baadhi ya wachungaji na waumini wa dayosisi hiyo walipingwa kwa madai kwamba taratibu hazikufuatwa kwa kuwa chombo cha mwisho kufanya uamuzi wa aina hiyo nji Mkutano Mkuu wa Dayosisi pekee.

Kutokana na mgogoro huo, Halmashauri Kuu ya KKKT chini ya Mkuu wa Kanisa, Askofu Dk. Shoo, iliunda Kamati Maalum kwa ajili ya kusuluhisha na kuumaliza ikiwa chini ya Askofu Dk. Alex Malasusa wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani. Wajumbe wengine walikuwa Askofu Blaston Gaville wa Dayosisi ya Iringa na Askofu Amon Kinyunyu wa Dayosisi ya Dodoma.

Baada ya vikao kadhaa vya usuluhishi, upande wa Mwaikali ulikubali kurejesha kiti cha uaskofu Tukuyu lakini haukufanya hivyo na hatimaye ulifikiwa uamuzi wa kufikishwa suala hilo kwenye Mkutano Mkuu wa Dayosisi kwa hatua zaidi.

Dk. Mwaikali na timu yake hawakuhudhuria mkutano huo uliofanyika Uyole na hatimaye wajumbe kupiga kura ya kutokuwa na imani naye na kufanya uchaguzi mkuu uliompata Mchungaji Mwakihaba kuwa Askofu Mteule na Mchungaji Dk. Njinga kuwa msaidizi wake.

## Shaka akemea urasimu wa viongozi serikalini

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, ameiagiza serikali ya mkoa wa Mtwara kuacha urasimu kwa kuchelewesha ugawaji wa pembejeo kwa wakulima wa korosho mkoani humo.

Pia amemwagiza Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Meja Jenerali Michael Gaguti, kuunda timu maalumu itakayoshirikisha vyombo vya ulinzi na usalama katika mkoa kuchunguza sababu ya kukwama kwa baadhi ya miradi ya maji wilayani Nanyumbu ukiwamo Nandete ambao umeonekana kuwa pasua kichwa.

Shaka alitoa maagizo hayo baada ya kuwasili Mkoa wa Mtwara kwa ziara ya kikazi akitokea mkoani Lindi. Baada ya kufika Mtwara, alipata nafasi ya kusikiliza kero za wananchi.

Katika kero hizo, wananchi hao walilalamikia kutokupata pembejeo hali inayowapa wasiwasi kwamba huenda wakachelewa kwenye maandalizi ya kilimo cha korosho kuelekea msimu mpya.

Baada ya kusikiliza malalamiko hayo, Shaka aliitaka serikali ya mkoa wa Mtwara ihakikishe inagawa pembejeo za kilimo mara moja kwa kuwa hakuna sababu ya kuzichelewesha wakati Rais Samia alishazitoa na zilishafika mkoa huo.

"Tumetoka asubuhi tumezungumza na Mkuu wa Mkoa. Taarifa ambayo nimepatiwa ni kwamba pembejeo zimeshafika, hivyo niombe serikali ya mkoa kuacha urasimu. Ndani ya wiki moja pembejeo ziwe zimetoka. Tunataka wananchi wanufaike na uwepo wa Rais Samia (Suluhu Hassan) ambaye ameamua kutoa bure pembejeo za kilimo kuhakikisha wakulima wananufaika na kilimo," alisema Shaka.

Kuhusu miradi ya maji ambayo Shaka ameitembelea na kukagua ujenzi wake, alitumia nafasi hiyo kutoa maagizo kwa mkuu wa mkoa kufanya uchunguzi kwa kutumia vyombo vya ulinzi na usalama baada ya kubainika uwapo wa mradi wa maji Nandete ambao unasuasua wakati wananchi wakikabiliwa na uhaba wa maji.

Akizungumza na wananchi katika Kijiji cha Mnanje, wilayani Nanyumbu, Shaka alisema anazo taarifa za kutosha za mradi wa maji Nandete, hivyo ametaka kupata majibu kabla ya kuondoka Mkoa wa Mtwara.

"Nimepokea malalamiko mengi sana kuhusu huu mradi wa maji Nandete. Serikali ya Rais Samia na CCM itasimama na wananchi," alisema Shaka.

"Hatuwezi kuona watu wachache ambao wanaangalia maslahi yao binafsi wanakwamisha miradi ya maji. Huu mradi wa maji Natende nataka majibu yake na mkuu wa mkoa tumia vyombo vyako kupata taarifa na bahati nzuri taarifa zote ninazo. Kuna mambo mengi yamefanyika na hawasemi, kuna mambo mengi yamejificha," alisema Shaka.

# NIMR yaja na mbinu kuzikabili athari VVU

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya Taifa na Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) imeshauri mazoezi ya mwili yawe sehemu ya tiba katika kliniki za watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) baada ya utafiti kuonyesha kuwa tatizo la ugonjwa wa kisukari ni kubwa kwao kuliko wasiokuwa na maambukizo.

Mkurugenzi Mkuu wa NIMR, Prof. Yunus Mgaya, aliyasema hayo juzi jijini hapa kwenye mkutano wa kutoa matokeo ya utafiti wa ugonjwa wa kisukari kwa watu wenye VVU jijini Mwanza kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Copenhagen cha Denmark.

Alisema utafiti huo uliowashirikisha watu 2,000 na kufanyika kuanzia mwaka 2016 hadi 2022, washiriki waoishi na VVU walipatikana katika vituo vya afya vya Buzuruga, Igoma na Kisesa pamoja na Hospitali za Nyamagana na Seko-Toure.

"Kufanya mazoezi ya mwili ya kutumia nguvu kiasi kwa viwango vinavyoshauriwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa takribani dakika 150 hadi 300 kwa wiki, kunapunguza uwezekano wa kupata ugonjwa wa kisukari kwa asilimia 60," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema ufanyaji wa mazoezi ya mwili unaongeza ufanisi wa kongosho na seli zake katika kutoa insulin ili kupunguza hatari ya ugonjwa wa kisukari kwa watu wenye VVU.

"Watu wanaoishi na VVU wanafanya mazoezi kidogo kulinganisha na watu wasiokuwa na VVU, ugonjwa wa sukari unaongeza hatari ya kupata ugonjwa figo, pia matokeo mengine yaliyopatikana kwenye utafiti ni uzito mkubwa na unywaji pombe kupitiliza vinaongeza hatari ya kupata ugonjwa wa figo," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema utafiti huo ulihusisha watu wazima wanaoishi jijini Mwanza wenye sifa mbalimbali ikiwamo za watu wanaoishi na VVU ambao hawajaanza dawa za kupunguza makali ya VVU, watu wanaoishi na VVU ambao wanatumia dawa za kupunguza makali ya VVU na watu wasiokuwa na VVU.

Kadhalika, alisema utafiti ulihusisha wilaya za Nyamagana, Ilemela na Magu ambako ulibaini kuwa tatizo la ugonjwa wa kisukari ni kubwa kwa watu wenye maambukizo ya VVU kuliko wale wasiokuwa na maambukizi ya VVU.Prof. Mgaya alisema walibaini tatizo la ugonjwa wa figo ni kubwa miongoni mwa watu wazima wanaoishi na VVU.

"Tunapendekeza huduma za matibabu ya kisukari ziunganishwe kwenye kliniki za watu wanaoishi na VVU, elimu ya kufanya mazoezi itolewe kwa msisitizo kwenye vituo vya afya hasa kwa watu wanaoishi na VVU, hatua za kubaini tatizo la figo zifanyike mapema na watu wanaoishi na VVU wachukue tahadhari za kujikinga na kisukari," alisema.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Seif Shekilaghe, alisema wizara itaendelea kuipatia fedha za utafiti NIMR ili kupata majibu mazuri na kuondoa matatizo hayo kwa jamii.

Awali, Mtafiti wa Mkuu katika utafiti huo kutoka NIMR, Dk. George Praygod, alibainisha kuwa katika nchi za Afrika kulionekana hakuna takwimu zinazowashawishi watunga sera kubadili sera ili kuhakikisha huduma za magonjwa yasiyoambukiza, kuunganishwa na VVU.



Meneja Rasilimali Watu wa Kampuni ya The Guardian Ltd inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Emmanuel Matondo (wapili kushoto), akikabidhi zawadi ya pesa taslimu kwa mwandishi wa habari wa kampuni hiyo, Jenifer Gilla, katika ofisi za TGL Mikocheni, Dar es Salaam jana, baada ya kushinda Tuzo za Umahiri za Uandishi wa Habari (EJAT) 2021 mapema wiki hii. Jumla ya waandishi 12 wa TGL walioshinda tuzo hizo walizawadiwa. Kushoto Mhariri Mtendaji wa Gazeti la The Guardian, Wallace Maugo na Mhariri Msaidizi wa gazeti la Nipashe, Epson Luhwago. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Baraza lasimamisha mabadiliko tozo usafi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

BARAZA la Manispaa Mjini Zanzibar limesema mabadiliko ya tozo ya ada ya usafi yaliyofanywa na Kampuni ya Usafi ya Vigors Clean Ltd, yamefanyika kinyume cha sheria na kanuni za Baraza la Mji Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Malindi, Mkurugenzi wa Baraza hilo, Ali Khamis Mohamed, alisema baraza limeshtushwa na mabadiliko ya ada kupanda kutoka Sh. 135,000 mpaka 500,000 kuanzia Julai, mwaka huu, katika migahawa na hoteli bila baraza kushirikishwa.

"Tumepokea mabadiliko ya tozo za ada za usafi yaliyofanywa na Kampuni ya V- Clean kupitia mitandao ya jamii. Bahati mbaya wamefanya bila kutushirikisha na hii ni kinyume cha sheria na kanuni za Baraza la Mji," alisema.

Kwa msingi huo, alisema mabadiliko yaliyofanyika hayatambuliki na tayari hatua za kuiandikia barua kabla ya kufanyika kikao cha pamoja zimefanyika. Aliwataka wawekezaji na wafanyabiashara kuendelea kuwa na utulivu wakati Baraza la Manispaa likiendelea kutafuta ufumbuzi.

Ali alisema kwa mujibu wa Kanuni zilizotungwa mwaka 2020 na kuchapishwa katika gazeti la serikali, hoteli za kati zinatakiwa kulipa ada ya usafi ya Sh. 50,000, vizimba vya biashara sokoni Sh. 6,500 na nyumba za kawaida Sh. 3,000 wakati hoteli za daraja la juu zikitakiwa kulipa Sh. milioni 1.5 kwa mwezi. Mkurugenzi huyo alisema kutokana na kuwapo kwa utitiri leseni na tozo za ada katika maeneo ya huduma za jamii, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussen Ali Mwinyi, aliagiza kuwekwa mfumo mmoja wa tozo za ada ili kuleta unafuu kwa wananchi na kwa watoa huduma Zanzibar.

Wakizungumzia mabadiliko hayo, wamiliki wa hoteli na wawekezaji walisema serikali inapaswa kuingilia kati ili kuokoa sekta ya utalii Zanzibar pamoja na wafanyabiashara.

"Ukweli tozo za ada zilizopangwa zinaumiza sana wawekezaji na wafanyabiashara. Haiwezekani ada ya usafi inapandishwa kutoka Sh. 135,000 mpaka 500,000 kwa mwezi mbali na kodi nyingine tunazolipa kila mwezi," alisema mmiliki wa hoteli ya Rumaisa, Mohamed Abdulrahman Bajubeir.

Bajubeir alisema pamoja na huduma za usafi kubinafsishwa na kusimamiwa na kuendeshwa na kampuni binafsi, bado huduma zinazotolewa si za kuridhisha kutokana na upungufu wa vifaa na wafanyakazi kulazimika kubeba taka katika viroba na kukusanya kwa maboksi.

Kiongozi Mwandamizi wa Hoteli ya Mizingani Sea Front, Zubeda Mussa, alisema wakati umefika kwa serikali kuingilia kati mgogoro wa tozo za usafi ili kunusuru sekta za biashara na utalii.

Mabadiliko hayo ya tozo za ada ya usafi yamekuja siku chache tangu kampuni ya Vigors Clean kutakiwa kulipa Sh. milioni 63 na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Zanzibar baada ya msamaha wa kodi ya magari mawili ya kuzoa taka kukataliwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Naibu Kamishna wa TRA Zanzibar, Juma Bakary, alisema magari hayo yaliingizwa Oktoba 27, mwaka jana, kupitia Bandari ya Malindi na kutolewa kwa dhamana ya bodi wakati wakiendelea kukamilisha maombi ya msamaha wa kodi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kabla ya kukataliwa na waziri.



Meneja wa Benki ya CRDB Kanda ya Dar es Salaam, Badru Idd (kushoto), akimkabidhi tuzo Meneja Lojistiki wa Benki ya CRDB, Savio Fernandes, kwa kutambua mchango wake katika kukuza biashara ya benki hiyo Kanda ya Mashariki, hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Nesi adaiwa kukamatwa na dawa za kulevya

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ( DCEA) imesema katika kipindi cha Januari hadi Mei mwaka huu, imekamata kilo 877.217 za dawa za kulevya, kuzuia uingizaji wa kilo 122,047.0855 na lita 85 za kemikali bashirifu nchini.

Vilevile, mamlaka hiyo imesema kumkamata nesi kutokana na kudaiwa kuwa na kiwango kikubwa cha dawa za kulevya aina ya heroine.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Gerald Kusaya, alitoa takwimu hizo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu operesheni waliyoifanya ya ukamataji wa dawa za kulevya katika kipindi cha miezi mitano.

Kamishna Jenerali Kusaya alisema kati ya kiasi hicho cha dawa za kulevya walichokamata heroine ni kilo 174.122 zilizowahusisha watuhumiwa sita ambao kwa sasa wameshafikishwa mahakamani.

"Mei 12, mwaka huu, katika eneo la Tabata Relini, Wilaya ya Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam, mamlaka ilikamata kilo 174.77 za dawa za kulevya aina ya heroine. Katika tukio hilo, Salum Mpangula alikamatwa kwa tuhuma za kusafirisha dawa hizo," alisema.

Alidai kuwa kufuatia upekuzi iliofanyika nyumbani kwa mtuhumiwa huyo ambaye ni nesi wa moja ya vituo vya afya jijini, paketi 162 range unga uliodhaniwa kuwa dawa za kulevya zilikutwa ndani ya viroba sita vilivyokuwa vimehifadhiwa chumbani kwake huku paketi moja ikiwa imewekwa kwenye mfuko mweusi na kufichwa chini ya kitanda.

Alifafanua kuwa taarifa za kiuchunguzi wa kitaalamu kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali zilithibitisha kuwa paketi zote 163 zilikuwa na dawa za kulevya aina ya heroine.

Kuhusu kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya, alisema DCEA inaendelea kufanya ukaguzi wa kufuatilia watu wanaokiuka taratibu za uingizaji na usambazaji.

Alisema katika kipindi cha Januari hadi Mei mwaka huu DCEA kupitia mfumo wa kielektroniki ilifanikiwa kuzuia uingizaji wa kilo 122,047.085 na lita 85 za kemikali bashirifu.

Pia alisema katika kipindi hicho, DCEA imeteketeza ekari 21 za mashamba ya bangi mkoani Arusha na kilo 250.7 za dawa za kulevya aina ya heroine na cocaine ambazo mashauri yake yalimalizika mahakamani.

Kamishna Jenerali Kusaya alisema: "Katika kuhakikisha jamii inapata elimu sahihi juu ya tatizo la dawa za kulevya, DCEA imeandaa mwongozo utakaotumika kutoa elimu, imeshiriki kuandaa ujumbe juu ya tatizo la dawa za kulevya katika mbio za Mwenge wa Uhuru zinazoendelea na kutoa elimu kwa kamati za ulinzi na usalama, kamati za afya na watendaji wa serikali za mitaa ili wasaidie kuongeza uelewa wa tatizo la dawa za kulevya kwa jamii."

# Kishindo cha Utalii

**Romana Mallya**, DODOMA

WIZARA ya Maliasili na Utalii imeliomba Bunge kuidhinishia Sh. bilioni 624.142 ili kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Katika mwaka huu wa fedha, wizara hiyo iliidhinishwa Sh. bilioni 571.632 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake.

Akiwasilisha jana bungeni jijini hapa makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wake, Balozi Pindi Chana, alisema filamu ya Tanzania The Royal Tour iliyoandaliwa na serikali na kuchezwa na Rais Samia Suluhu Hassan, imeleta neema kwa sekta ya utalii.

"Programu hii ambayo mwezi Aprili mwaka huu ilizinduliwa New York na Jiji la Los Angeles na baadaye Arusha, Zanzibar, Dar es Salaam na Dodoma, imetambulisha Tanzania kimataifa kwa kutangaza vivutio vya utalii vya kipekee vya nchi yetu, kuonyesha fursa mbalimbali za uwekezaji sekta ya maliasili na utalii pamoja na kuimarisha nafasi ya nchi kimataifa.

"Programu hii imeanza kuleta matunda kwa kuvutia watalii na wawekezaji mbalimbali kutembelea nchini. Wakala wa utalii zaidi ya 30 kutoka katika masoko ya utalii yakiwamo Marekani, Ufaransa na Lithuania wamehamasika kutembelea nchini ili kujifunza na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii na kuitangaza nchi," alisema.

Waziri huyo alisema wawekezaji kutoka Bulgaria wameonyesha nia ya kuwekeza kwa kujenga hoteli nne zenye hadhi ya nyota tano katika Hifadhi za Taifa Serengeti, Ziwa Manyara na Tarangire na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA).

Pia alisema serikali imetia saini mkataba wa ushirikiano katika suala la utalii, biashara na uwekezaji baina ya Tanzania na Jiji la Dallas, Marekani Aprili mwaka huu, ambapo hatua hiyo itafungua fursa za usafiri wa moja kwa moja za ndege kutoka Tanzania hadi Dallas na kwamba hiyo itaongeza idadi ya watalii.

**VITA DHIDI YA UJANGILI**

Waziri huyo alisema wizara imeendelea kuongeza jitihada za kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa rasilimali na kudhibiti ujangili, biashara haramu za nyara na uvunaji haramu wa mazao ya misitu na nyuki na uvamizi wa maeneo yaliyojifadhiwa.

Alisema jitihada hizo zinadhihirishwa na sensa ya wanyamapori iliyofanyika mwaka 2021 ambapo idadi ya tembo imeongezeka kwa asilimia 30 katika mfumo Ikolojia Ziwa Natron-West Kilimanjaro.

"Ikolojia ya Ruaha-Rungwa nyati wameongezeka kwa asilimia 80, pundamilia asilimia 36 na palahala asilimia 65 kulinganishwa na sensa iliyofanyika mwaka 2018.

"Idadi ya faru weusi ambao wako hatarini kutoweka imeongezeka kwa asilimia 27.5 kulinganishwa na idadi yao kwa mwaka 2018. Ongezeko la wanyamapori hao ni kiashiria cha kuimarisha kwa ulinzi na usimamizi wa maeneo ya hifadhi," alipongeza.

Alisisitiza kuwa mafanikio hayo yamechangiwa na juhudi za serikali ikiwa ni pamoja na kufanya doria ambapo jumla ya siku doria 434,371 zimefanyika na kuwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 7,719 pamoja na nyara za serikali na magogo yenye ujazo wa mita 1,218.

Pia alisema operesheni maalum za kiintelijensia zilizowezesha kuzuiwa kwa matukio 66 ya ujangili, kukamatwa bunduki 135 na kuvunjwa kwa mtandao wake.

**GPS WANYAMAPORI**

Waziri Chana pia alisema wizara katika kutatua migogoro baina ya binadamu na wanyamapori, jumla ya tembo 107 (Ngorongoro, Tarangire na Selous, mapori ya akiba Naswa na Ikorongo na pori Tengefu Longido, mbwa mwitu saba, faru 64 na simba 21 (wa Serengeti na Ruaha) waliofungwa mikanda ya mawasiliano (GPS Collar) wameendelea kufuatiliwa mienendo yao na kutoa mafunzo katika wilaya 21 na kujenga vizimba viwili vya mamba Ziwa Rukwa.

Alisema serikali imetenga Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa vituo 11 vya askari wa kuwazuia katika wilaya 11 na kwamba hadi Aprili mwaka huu, Sh. milioni 790.7 zimetolewa kwa waathrika 3,598 katika wilaya 36.

Waziri Chana alisema tathmini zilizofanyika katika hifadhi za taifa nane za Serengeti, Arusha, Saadan, Mkomazi, Mikumi, Katavi, Nyerere na Ibanda pamoja na NCAA imebaini spichi 33 za mimea vamizi kwenye hekta 35,331 na jumla ya hekta 10,668.88 zimedhibitiwa.

**SULUHU NGORONGORO**

Alisema ili kutafuta suluhu ya kudumu ya matumizi mseto ya ardhi eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kaya 278 zenye wakati 1,439 walikuwa wamejiandikisha kuhama na wizara imebainisha maeneo ya Handeni (Tanga) na Kitwai (Manyara) kwa ajili yao.

"Hadi Aprili mwaka huu, wizara ilipima eneo lenye ukubwa wa hekta 73,528.73 lililogawanywa kwa ajili ya matumizi mbalimbali yakiwamo; makazi (hekta 10,080.4), kilimo (hekta 13,628.48), malisho (hekta (22,176.06), ujenzi wa taasisi za elimu ya juu na vyuo (hekta 1,329.37) ushoroba wa wanyamapori (hekta 26,314.42) na hifadhi ya misitu (hekta 6,082.72)," alisema.

Alisema upimaji na upangaji wa matumizi ya ardhi eneo lililobaki pamoja na Kitwai lenye ukubwa wa hekta 409,416 linaendelea.

Pia alisema wizara kwa kushirikiana na uongozi wa mkoa wa Arusha na Tanga imekamilisha ujenzi wa nyumba za makazi 103 Handeni kati ya 500 zitakazojengwa kwa ajili ya watu waishio ndani ya hifadhi Ngorongoro.

**WATALII WAONGEZEKA**

Waziri Chana alisema UVIKO-19 umeendelea kuwa stahimilivu ambapo idadi ya utalii imeongezeka kutoka 620,867 (2020) hadi 922,692 (2021) ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 48.6 na mapato ya watalii kimataifa imeongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 714.59 (2020) hadi Dola milioni 1310.34 (2021) sawa na ongezeko la asilimia 82.

Alisema utalii wa ndani umekua kutoka 562,549 (2020) hadi 788,933 (2021) sawa na ongezeko la asilimia 40.2 na kwamba wizara imefanikiwa kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea vituo vya malikale na makumbusho kutoka 349,264 (2020) hadi 582,264 (2021) sawa na ongezeko la asilimia 167.

**TUZO**

Waziri huyo alisema Hifadhi ya Taifa Serengeti imeibuka kinara kati ya vivutio 10 bora vilivyoorodheshwa na mtandao wa safari bookings.com ulio maarufu duniani kama kivutio kinachofaa kutembelewa katika Bara la Afrika.

"Shirika la Hifadhi za Taifa limetunukiwa cheti cha ubora wa huduma za kiwango cha kimataifa cha ISO 9001:2015 kutokana na kuimarishwa kwa utoaji wa huduma bora za utalii na Zanzibar na Jiji la Arusha zimeorodheshwa na Tripadvisor kupitia Travellers Choise Destination-Afrika kuwa miongoni mwa maeneo 10 ya shughuli za utalii barani Afrika," alisema.

**VIPAUMBELE 2022/23**

Alisema kuwa katika mwaka ujao wa fedha, wizara itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele mbalimbali vya sekta ambavyo ni pamoja na: Kukuza utalii wa ndani; kuongeza kasi ya utangazaji utalii kitaifa na kimataifa kwa kuendeleza programu ya The Royal Tour; na kuibua masoko mapya ya utalii.

"Kukarabati na kuimarisha miundombinu katika maeneo ya hifadhi; na kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati ikiwamo utalii wa fukwe; mikutano na matukio; meli za kitalii, michezo na utamaduni.

"Vipaumbele vingine ni kuendelea kuishirikisha jamii katika mbinu za kujikinga dhidi ya wanyamapori hatarishi; kuimarisha shughuli za upandaji miti, ufugaji nyuki na mnyororo wa thamani wa mazao yake; kuimarisha mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu; kuimarisha mfumo wa utoaji huduma za utalii ili kukidhi viwango vya kimataifa na kuboresha ulinzi na usalama wa rasilimali za maliasili na malikale," alisema.

Waziri huyo alivitaja vingine ni kuendelea kuimarisha utafiti pamoja na mifumo ya takwimu na ukusanyaji wa mapato ya serikali yatokanayo na sekta ya maliasili na utalii na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na kuendeleza rasilimali watu.

**KAMATI YA BUNGE**

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Shaban Shekilindi, akisoma taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya wizara hiyo, alisema:

"Kamati ina maoni kwamba uwekaji wa malengo ya ukusanyaji wa maduhuli unaweza kuleta tija iwapo utazingatia uhalisia vinginevyo wizara itakuwa na malengo ambayo hayatekelezeki.

"Kamati inaishauri serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha zote za maendeleo na kwa wakati ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ambayo pia yanaendana na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 inayosisitiza katika kuongeza na kukuza wigo wa bidhaa/mazao ya utalii ili kufikia watalii milioni tano ifikapo mwaka 2025."

Pia alisema kamati hiyo inaitaka serikali ichukue hatua madhubuti na za haraka katika kukabiliana na matatizo ya migongano ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu kama vile tembo, mamba, tumbili na wengineo ili kuondoa madhara yanayoendelea kujitokeza dhidi ya binadamu bila ya kuathiri uwapo wa wanyama hao.

■SOMA HOTUBA UK. 11-15

# Serikali yachukua hatua wimbi la tano UVIKO-19

Na Beatrice Shayo

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema serikali imeanza kuchukua hatua ya kukabiliana na wimbi la tano la ugonjwa wa UVIKO-19 kutokana na nchi za jirani kuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa.

Vilevile, amebainisha kuwa Mkoa wa Ruvuma unaongoza kwa chanjo huku Mkoa wa Manyara ukishika mkia.

Waziri Ummy alibainisha hayo juzi jijini Dar es Salaam alipozindua Mpango wa Marekani wa Upatikanaji wa Chanjo (Global Vax) wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 25 (Sh. bilioni 58) utakaowezesha upatikanaji wa chanjo.

"Mpaka hivi sasa, Tanzania imepitia mawimbi manne ya maambukizi ya UVIKO-19 na serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa ugonjwa huu duniani ikiwamo katika mataifa yaliyoko barani Afrika na kuimarisha hatua stahiki zinazoshauriwa kitaalamu katika kukabiliana na janga hili," alisema.

Waziri huyo alisema ufuatiliaji wa takwimu za maradhi hayo katika mataifa mbalimbali umebaini kwa kipindi cha wiki tano zilizopita kuna ongezeko la wagonjwa katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) hususan nchi ya Afrika ya Kusini ambayo imeripoti visa vipya 186,254 kulinganishwa na wiki nne zilizotangulia ambapo kulikuwa na visa 47,429.

Alisema kutokana na mwingiliano wa kibiashara baina ya nchi hizi, hakuna budi kuongeza juhudi na jitihada za kusimamia afua za kukabiliana na ugonjwa huo kwa kuwa Tanzania inaweza kuwa kwenye hatari ya kukumbwa na wimbi la tano.

Alisema kutokana na juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau, kasi ya maambukizi ya UVIKO-19 imeendelea kupungua nchini.

Alisema tangu ugonjwa huo uingie nchini Machi 16, 2020 hadi kufikia Mei 20, 2021, jumla ya watu 34,002 wamethibitika kuambukizwa huku 803 wakipoteza maisha. Waziri Ummy alisema Tanzania inaungana na nchi nyingine duniani kuhakikisha inaendelea kutekeleza mikakati madhubuti ya kujikinga na kukabiliana na ugonjwa huo.

"Tangu uzinduzi huo, serikali imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuimarisha utoaji wa chanjo dhidi ya UVIKO-19 nchini ambapo baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuongeza vituo vya kutolea huduma za chanjo kutoka vituo 550 mwezi Julai, 2021 wakati tunaanza kutoa chanjo hizi hadi kufikia vituo 7,000 hivi sasa," alisema.

Alibainisha kuwa hadi kufikia Mei 24, mwaka huu, zaidi ya dozi 13,400,000 za chanjo zilikuwa zimepokewa kutoka vyanzo mbalimbali na kusambazwa kwa ajili ya matumizi nchini.

"Tumebaini kuwa baadhi ya walengwa waliopata dozi ya kwanza ya chanjo zinazotolewa kwa dozi mbili hawarudi kupata dozi ya pili.

"Mathalani, kwa kipindi cha mwezi Februari, 2022, wateja ambao hawakurudi kupata dozi ya pili ya chanjo aina ya Sinopharm ni 308,164 asilimia 25, chanjo aina ya Pfizer ni 147,345 asilimia 36 na chanjo aina ya Moderna ni 161,580 asilimia 24," alisema.

Balozi wa Marekani nchini, Dk. Donald Wright, alisema mpango huo unalenga kuongeza kasi ya upatikanaji wa chanjo na kuisaidia serikali kufikia malengo ya asilimia 60 ya walengwa.

Alisema Marekani imejitolea kuisaidia Tanzania katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo, hivyo ni jukumu la kila mmoja kuhakikisha anapata chanjo ili awe salama.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, alisema wagonjwa waliopo katika hospitali ambao wamebainika kuugua ugonjwa huo ni wale ambao hawajachanja, hivyo ni muhimu wananchi wakachanja ili wawe salama.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kulia) na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Stanbic, Kevin Wingfield, wakipanda mti baada ya benki hiyo kukabidhi madawati 200 yenye thamani ya Sh. milioni 20 kwa ajili ya shule za sekondari za Lejico, Lufiyo na Mshewe mkoani Mbeya hivi karibuni, ikiwa ni sehemu ya mpango unaoendelea wa benki hiyo wa Madawati Initative, unaokusudia kuchangia madawati kwa shule za serikali mbalimbali nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kisena, mkewe waachiwa huru

Na Grace Gurisha

ALIYEKUWA Mkurugenzi wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (Udart), Robert Kisena na mkewe Frolencia Mashauri, wameachia huru na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu katika kesi ya uhujumu uchumi iliyokuwa inawakabili baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuwasilisha nia ya kutokuendelea kuwashtaki.

Mahakama hiyo pia imetoa amri kwamba kama upande wa Jamhuri wana nia ya kuwashtaki tena kwa makosa hayo hayo, wasiwakamate hadi upelelezi ukamilike.

Amri hiyo ilitolewa jana Hakimu Mkazi Mkuu Rita Tarimo wa mahakama hiyo baada ya Wakili wa Serikali kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Pendo Temu, kuwasilisha nia ya DPP ya kutokuendelea kuwashtaki.

Temu alidai kuwa DPP alishauri kuiondoa kesi hiyo mahakamani kwa mujibu wa sheria.

"Mahakama inakubaliana na nia ya DPP. Kwa hiyo, inawaachia huru washtakiwa wote, lakini kama mnataka kuwashtaki tena na makosa haya haya, basi msiwakamate tena hadi upelelezi ukamilike," Hakimu alitamka.

Mbali na Kisena na mkewe Florencia, washtakiwa wengine ni Kulwa Kisena, Charles Newe na Chen Shi, ambapo Kisena na Kulwa hawakwenda nyumbani kwa sababu wana kesi nyingine ya uhujumu uchumi ambayo haina dhamana.

Kesi hiyo iliondolewa na DPP baada ya washtakiwa kukaa miaka mitatu bila upelelezi kukamilika. Washtakiwa hao walikuwa wanatetewa na Wakili Nehemiah Nkoko.

Kisena na wenzake walikuwa wanakabiliwa na mashtaka 15, yakiwamo ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kuisababishia Udart hasara ya Sh. 2,414,326,260.70 (Sh. bilioni 2.4).

Inadaiwa kuwa kati ya Oktoba 2012 hadi Mei 31, 2018, washtakiwa wanadaiwa kutenda makosa hayo. Inadaiwa kati ya Januari Mosi, 2011 na Mei 31,2018 katika mahali tofauti, wakiwa na watu wengine, waliratibu shughuli za kihalifu huku wakijua kufanya hivyo ni kosa la kisheria.

Inadaiwa kati ya Januari Mosi, 2015 na Desemba 31,2017 katika eneo la Jangwani, washtakiwa hao wakiwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Zenon Oil Gas Limited, walijenga kituo cha mafuta kinachoitwa. Zenon Oil and Gas katika karakana ya Kampuni ya Udart bila ya kuwa na kibali kutoka Mamlaka ya Uthibiti wa Huduma na Nishati na Maji (EWURA).

# MOI yasambaza ujuzi wake mikoani

Na Mary Geofrey

TAASISI ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI) kwa kushirikiana na Kampuni ya Smart Toch Solution ya nchini Misri, imefanya mafunzo ya kutibu mifupa mirefu ya miguu, mikono na kiuno kwa madaktari wa wilaya na mikoa nchini.

Mafunzo hayo yamefanyika kwa siku mbili MOI jijini Dar es Salaam kwa lengo la kuwajengea uwezo madaktari kutumia njia za kisasa za kutoa matibabu kwa kuweka vyuma kwa njia bora.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kufunga mafunzo hayo, alisema wameingia mkataba wa miaka mitatu wa kutoa mafunzo kwa madaktari na wauguzi nchini Misri ili waende wakajifunze.

Alisema mafunzo hayo yatasaidia huduma ya upasuaji kwa majeruhi wa ajali kufanyika katika hospitali za wilaya na mikoa nchini.

"Tunatekeleza maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kutoa huduma bora za matibabu," mkurugenzi huyo alisema.

Pia alisema mafunzo hayo yamelenga madaktari kutoka mikoa yote nchini kutoka Ghana, Sudani ya Kusini na Uganda.

Alisema mifupa mirefu ya mikono, miguu na kiuno inavunjika kwa sababu mbalimbali ikiwamo ya ajali za magari, wanaodondoka kwenye miti na wanaoanguka michezoni.

Dk. Boniface alisema tofauti na tiba ya awali ya kufunga mawe ambayo ilichukua zaidi ya miezi miwili hadi mitatu kupona lakini tiba hiyo inachukua mwezi mmoja kupona.

Alisema kwa siku hospitalini hapo wanapokea majeruhi 10 hadi 15 wa ajali za bodaboda ambao ndiyo wavunjika mifupa mikubwa.

Daktari Bingwa wa Mifupa wa MOI, Dk. Rabi Ndesarua, alisema mafunzo hayo ya siku mbili yamedhaminiwa na MOI na Kampuni ya Smart Toch Solution ya nchini Misri.

Alisema mafunzo hayo yatawasaidia madaktari kujenga uwezo wa kuelewa namna ya kutibu mifupa katika taasisi na nje ya taasisi.

Alisema pia wamepata vifaa mbalimbali vya mafunzo na kutibu wagonjwa.

"Kabla ya mafunzo wagonjwa wengi walikuwa wanatoka hospitali za mikoa na wilaya kuja MOI kupata matibabu, kutumia muda mrefu, gharama kubwa lakini baada ya mafunzo watatibiwa huko huko," alisema Dk. Ndesarua.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la heri Taifa Stars

**TIMU** ya Taifa ya Soka ya Tanzania, Taifa Stars, leo usiku itatupa karata yake ya kwanza kwenye kinyang'anyiro cha kuwania kusaka tiketi ya kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) nchini Ivory Coast mwakani, ikicheza na Niger.

Mchezo huo utapigwa kwenye Uwanja wa L'amitie jijini Cotonou nchini Benin kutokana na Niger viwanja vyake kutokidhi vigezo vya Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Stars inaingia kwenye mchezo huo ikiwania kuhakikisha inashinda ili kujiweka kwenye mazingira mazuri zaidi katika mechi nyingine za kundi lake la F.

Kama ambavyo nahodha wa timu hiyo, Mbwana Samatta alivyosema wakiwa wanaondoka nchini juzi kuelekea Benin kuwa wamejiandaa vizuri kupata ushindi ili kujiweka kwenye mazingira mazuri na morali ya kuendelea kufanya vizuri kwenye kundi lake, sisi pia tuna imani watafanya vizuri.

"Tunataka kuanza vizuri, na kwa bahati mbaya tunaanzia ugenini, lakini bahati nzuri pia ni kwamba iwapo tutashinda ugenini itakuwa imetupa morali kubwa ya kuendelea kufanya vizuri kwenye mechi zinazofuata," ilikuwa kauli ya Samatta wakati wakiondoka nchini.

Sisi tunajua kuwa mchezo huo hautakuwa rahisi kwa sababu hata Niger nao wanatamani kushiriki fainali za AFCON mwakani.

Hivyo ili kuhakikisha tunaipata nafasi hiyo, Stars lazima ipambane kwa nguvu zote kuhakikisha wanapata ushindi kwenye mchezo huo wa ugenini, ili watakapocheza hapa nyumbani iwe rahisi zaidi kwao.

Ikumbukwe kwamba, ukiwa unacheza ugenini unatakiwa kupambana kwelikweli kwa sababu ukipata matokeo mazuri ina maana kwamba, upo kwenye nafasi nzuri ya kufanya vyema zaidi nyumbani.

Hakuna kinachoshindikana kwa Stars kushinda ugenini, kwani wakati tukicheza kwenye michuano ya kufuzu Kombe la Dunia tulishinda mechi ugenini, kwa hiyo imetupa kujiamini kuwa tunaweza kushinda popote hata kwenye michuano hii.

Stars itakuwa inacheza kwenye uwanja iliouzoea kwani Oktoba 10, mwaka jana, ilicheza dhidi ya wenyeji Benin na kushinda bao 1-0 lililofungwa na Simom Msuva kwenye michuano ya kusaka tiketi ya kufuzu Kombe la Dunia litakalofanyika mwishoni mwa mwaka huu nchini Qatar.

Hivyo, Nipashe tunaimani kwamba, Stars haitakuwa mgeni sana wa uwanja huo hivyo inaweza kutumia mbinu walizotumia kwenye mchezo wa Oktoba 10, mwaka jana, kuweza kupata ushindi.

Stras ipo kundi F, pamoja na timu za Niger, Algeria, na Uganda ambazo zote sio za kubezwa, kwani zina wachezaji wakubwa na wenye uzoefu wa mashindano ya kimataifa, hivyo lazima wapambane kuhakikisha hawafungwi ugenini.

Stars ikifuzu michuano ya Afcon ya mwakani itayofanyika nchini Ivory Coast, itakuwa ni mara ya tatu, baada ya kufanya hivyo kwa mara ya kwanza mwaka 1980 na mara ya pili katika mashindano yaliyofanyika nchini Misri.

Hivyo kama uzoefu tayari Stars imeupata na hiyo maana yake ni kwamba, wanaweza kupambana vizuri na kupata ushindi kwenye mchezo huu wa kwanza na kujiweka kwenye mazingira mazuri kwa mechi zinazokuja.

Ushindi wa kwanza una faida kubwa kwa timu katika kuipa morali na kujiamini, hivyo kama Stars itapata ushindi kwenye mchezo wa leo, imani yetu ni kubwa kwamba, ina nafasi ya kusonga mbele kwenye mashindano haya makubwa zaidi barani Afrika kwa ngazi ya nchi.

Ombi letu kwa wachezaji ni kuzingatia maelekezo waliyopewa na benchi la ufundi pamoja na kutumia ufiti na utimamu wao walioupata kwenye mazoezi ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kushinda mchezo huo.

Hivyo, sisi tuna imani kubwa na Stars na inaweza kufanya vizuri na kuiwakilisha vyema nchi kwenye mashindano hayo ambayo yatafanyika kuanzia Juni 23 hadi Julai 23 mwakani.


Kila la kheri Taifa Stars.

**Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Taifa Stars.**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Pelekeni maoni ya kanuni, msije kulaumu

Na Adam Fungamwango

**TAYARI** Bodi ya Ligi imeanza mchakato wa kupokea maoni ya kuboresha kanuni za Ligi Kuu kwa ajili ya msimu ujao.

Kupitia mtandao rasmi wa Instagram wa Shirikisho la Soka nchini na Bodi ya Ligi, wamewataka wadau wote wa soka kutuma maoni kuhusu maboresho ya kanuni ili kuifanya iwe bora zaidi.

Ikataka mdau anayetaka kutoa mapendekezo ya maoni yake, au maboresho kutuma kwa barua pepe 'maoni@ligikuu.co.tz.'

Maoni hayo hupelekwa kwenye kamati husika kuchakatwa, kurekebishwa na hatimaye kupitishwa kwa ajili ya msimu husika.

Wakati Ligi Kuu msimu huu ukiendelea, baadhi ya mashabiki wa soka, wakiwamo hata baadhi ya viongozi wa klabu mbalimbali wamekuwa wakilalamika baadhi ya kanuni hasa pale zinapoanza kufanya kazi.

Hata hivyo, ni hao hao baadhi ya viongozi wa klabu ambao nao wanahusika kuziunda na kuzipitisha, lakini zinapoanza kuwagusa wanalalamika.

Tumekuwa tukiona viongozi, waandishi wa habari na wachambuzi wa masuala ya michezo wakilalamikia baadhi ya maamuzi yanayotolewa na Kamati ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ligi kwa madai kuwa hayakutenda haki, au yamepitwa na wakati.

Lakini kwenye nyakati kama hizi huwa watuwasikii wakipeleka maoni mapya, au kuhitaji marekebisho ya kanuni zilizopita.

Hiki ndiyo kipindi ambacho husikii wachambuzi au mashabiki wa soka wakihamasishana kupeleka maoni, lakini ngoja siku maamuzi ya adhabu yatoke kwa mujibu na kanuni ambazo zimeletwa, kuchakatwa na kupitishwa na kamati husika, ndipo mapovu yanapoanza kuwatoka.

Uzuri ni kwamba maoni anapeleka mtu yeyote, shabiki, mpenzi, mwandishi, mchambuzi, mdau, kiongozi wa soka na yoyote yule anayeguswa na mchezo huo. Hayabagui.

Huwa nashangaa sana wanavyokurupuka na kulalamika mtu anayefungiwa kujihusisha na soka miaka mitano kuwa ni mingi na imepitwa na wakati.

Lakini kwenye nyakati hizi za kupeleka maoni na maboresho kuwa soka letu kwa sasa limekuwa la kulipwa na makocha, viongozi kwa sasa hiyo ndiyo kazi yao inayowapatia kipato cha kuendesha maisha na familia zao, na si kama zamani soka lilikuwa la ridhaa, hivyo kumfungia mtu miaka mitano ni kama vile kumkamilisha ubaoni bila kazi yoyote, hivyo kuifanya familia yake iathirike.

Huu ndiyo wakati wa kupeleka maoni ya kurekebisha kanuni hiyo kuwa ni ya kizamani, enzi za soka la ridhaa ambapo soka ilikuwa ni burudani, kuleta mahusiano, upendo, mshikamano na afya, huku makocha, viongozi na wachezaji wakifanya kazi zingine kwenye makampuni mbalimbali.

Hivi karibuni tumeona jinsi Mbeya Kwanza ilivyonyang'anywa pointi kwa kulazimisha kutocheza mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Namungo kwa madai ya kuchelewa kwa gari la wagonjwa, ingawa inadaiwa lilikuja ndani ya muda.

Sasa ni wakati wa kupeleka mapendekezo ya maboresho kwa jinsi unavyoona kuwa kanuni hiyo haifai. Na kama inafaa gari inatakiwa iwe mwanzo wa mechi hadi mwisho isiondoke katikati na kurudi, au vyovyote unavyoona.

Nilimsikia Kocha wa Yanga, Nasreddine Nabi, akilalamika kuhusu kukatazwa kuchezesha wachezaji wote 12 wa kigeni waliosajiliwa kwenye Ligi Kuu, badala yake wanatakiwa kucheza nanane kwa mechi moja.

Si yeye tu, mashabiki wengi wanaipinga kanuni hiyo, huu sasa ndiyo wakati wake wa kwenda kupeleka maoni kuwa irekebishwe, wachezaji wote wanatakiwa waanze iwe wa kigeni wa wa kibongo bila ubaguzi.

Kuna faini za timu kupitia milango isiyohusika. Wengi wanalalamika, wanasema ni ndogo sama na ndiyo maana timu hazijali, zinaendelea tu na tabia hiyo.

Kinachotakiwa sasa ni kupeleka maoni ya kutaka faini iongezwe, ili timu ikipigwa, basi ijifikirie tena kurudia kosa.

Maoni yapo mengi sana kuhusu kanuni ambazo zimeonekana kuwa kero, lakini mashabiki na wachambuzi wamekuwa ni kama kawajui msingi wake umetokea wapi.

Ni kwamba wakati zinatumia haipaswi kulalamika, kwani watu wametoa maoni wakiwamo hao hao viongozi na makocha na zikapitisha.

Kanuni pekee ambayo inaonekana kutiliwa mkazo sana na hasa viongozi wa klabu za mikoani ni ile ya wao kuchukua mapato yote ya milangoni zikicheza na timu za Simba au Yanga.

Ndiyo maana hii ipo kwa misimu mitatu sasa, lakini zingine wanaziacha hadi pale zinapowachapa wenyewe ndipo wanaanza kupigia kelele watu.

Nawasihi wanamichezo wote kupeleka maoni ya mapendekezo ya kanuni mpya, au kuboresha zilizopo ili zitakazoanza kutumia msimu ujao zile ni zile zilizopendekezwa na wadau wenyewe na si vinginevyo.

Kama wanavyosema wenyewe Bodi ya Ligi ni kwamba, "Kanuni bora na rafiki huzaa ligi bora."

## Utafiti kufungua ubalozi Pakistan waanza rasmi

BUNGE limeelezwa kuwa serikali imeanza kufanya utafiti wa kuangalia uwezekano wa kufungua ubalozi nchini Pakistan.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Christine Ishengoma.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kufungua ubalozi wa Tanzania nchini Pakistan.

Akijibu swali hilo, Balozi Mbarouk, alisema utafiti huo unahusisha kuangalia faida za kiuchumi zilizoko nchini humo ambazo Tanzania itanufaika nazo ikiwa ni pamoja na kuainisha gharama za ufunguzi wa ubalozi huo na uendeshaji wake.

Katika swali lake la nyongeza, mbunge huyo alisema kwa kuwa nchi imefaidika kwenye uwekezaji, biashara na utalii kutokana na Balozi za Tanzania zilizoko kwenye nchi mbalimbali.

"Je, nchi hii ya Pakstani ambayo kuna ubalozi wake hapa nchini tunashirikianaje na nchi hii? Kuna nchi ngapi za namna hii ambazo zina balozi zao hapa nchini na sisi hatuna balozi kwenye nchi zao?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri huyo alisema pamoja na Tanzania kutokuwa na ubalozi Pakstani, Abu Dhabi na ushirikiano wa nchi hizo ni makubwa.

"Tumekuwa tukishirikiana masuala mbalimbali hasa ya kibiashara, tumekuwa tukisafirisha bidhaa kama pamba, chai, na madini ya vitu na nafaka kama vile maharage na kutoka Pakstani tumekuwa tukishirikiana nao na kuingiza bidhaa za dawa za binadamu, dawa za viwanda vya nguo na nafaka," alisema.

# Mbunge ahoji ruzuku vifaa ujenzi

MBUNGE wa Sikonge (CCM), Joseph Kakunda, amehoji kwa nini serikali haiweki ruzuku kwenye vifaa vya ujenzi ili wananchi wamiliki nyumba bora kwa kuwa asilimia 62.9 ya nyumba zilizoko nchini si bora.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alisema kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, kuna nyumba 11,873,950 na kati ya hizo, nyumba bora ni 3,444,519 sawa na asilimia 37.1 na nyumba 8,429,431 sawa na asilimia 62.9 si bora na kati ya hizo milioni 2,359,920 ni nyumba za nyasi.

"Nyumba ya kawaida ya vyumba viwili inahitaji Sh. 400,000 kununua bando mbili za bati, je, kwa nini serikali isiweke Sh. 200,000 kwa mtu kama ruzuku ili na yeye achangie Sh. 200,000 ili kuondoa kabisa nyumba za nyasi nchini," alihoji. Aidha, alisema kwa nini serikali isiweke viwango vya nyumba bora ili kila mtu awe anazingatia kiwango cha nyumba bora.

"Nyumba bora ya kuishi inatakiwa kuwa na sifa zipi nani kwa nini serikali haiweki ruzuku kwenye vifaa vya ujenzi ili kuwezesha wananchi kumiliki nyumba bora?" Alihoji.

Akijibu maswali hilo, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, alisema itakapokamilika sera ya nyumba na makazi matakwa ya mbunge huyo yatakuwa ndani ya sera.

"Wizara imeendelea kuandaa rasimu ya taifa ya nyumba ambapo pamoja na mambo mengine itatoa mwongozo wa nyumba bora inavyotakiwa kuzingatiwa na wadau wote, sera hiyo itaweka uratibu wa rahisi wa upatikanaji wa vifaa vya ujenzi kwa gharama nafuu, upatikanaji wa nyumba, mfumo wa wadau wa uratibu wa sekta ya nyumba na hivyo kuwezesha upatikanaji wa nyumba bora kuwa wa gharama nafuu," alisema. Awali, alisema nyumba ni mojawapo ya mahitaji muhimu ya mwanadamu.

"Nyumba bora ni ile yenye huduma bora kwa usalama na afya ya wakazi wake. Jitihada za serikali kuhakikisha nyumba bora zinajengwa kwa gharama nafuu ni pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya uanzishwaji wa viwanda vya kuzalisha vifaa vya ujenzi," alisema.

Pia alisema kufanya utafiti na kuwezesha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika kazi za ujenzi na kuhamasisha taasisi za fedha kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na ununuzi wa nyumba.



Naibu Waziri Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mbarouk Mbarouk, akijibu maswali yaliyoulizwa na baadhi ya wabunge katika mkutano wa saba kikao cha 37 cha Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kampuni mpya yaanza kununua tumbaku

SERIKALI imesema Kampuni ya Amy Holdings Limited imeanza ununuzi wa tumbaku na inataraji kununua tani 10,000 kwa msimu wa 2022/23.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Ushetu (CCM), Emmanuel Cherehani.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itakamilisha majadiliano na kampuni ya Tanzania Leaf Tobacco ili kurudi nchini kuendelea kununua tumbaku.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Mavunde alisema tumbaku hiyo itakayonunuliwa itachakatwa kwenye kiwanda kilichoko Morogoro ifikapo Julai, mwaka huu.

"Niwataarifu wakulima wa tumbaku nchini kuwa mwekezaji mpya ambaye ni mzawa kampuni ya Amy Holdings Limited amekamilisha taratibu za kuchukua shughuli zilizokuwa zinafanywa na Kampuni ya TLTC na ameshapewa leseni," alisema.


Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufungua milango ya wawekezaji ambayo matokeo yake ni pamoja na kupatikana kwa mwekezaji huyo.

"Serikali itaendelea kufungua milango ya wawekezaji kuja nchini kuwekeza kwenye zao la tumbaku na itaendelea kuweka mikakati ya kuhakikisha zao hili la tumbaku ili kupata wawekezaji na tumbaku ya wakulima inunuliwe,"alisema.

Hata hivyo, alisema wizara imetoa maelekezo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Tumbaku kukaa na wadau wote kuangalia namna bora ya uendeshaji wa biashara ya tumbaku ili wakulima wanufaike na tumbaku yao.

Kuhusu wakulima wanaodai kampuni ya Tanzania Leaf Tobacco, alikiri kuwapo kwa madai na kwamba Waziri (Hussein Bashe) alishawaita na kuwapa mwongozo wa malipo.

Alisema wamepewa hawatahuwisha leseni zao hadi pale watakapolipa madai ya wakulima.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# Wapaza sauti sheria kandamizi habari

**Na Mary Geofrey**

WADAU wa vyombo vya habari nchini kwa kushirikiana na Jukwa la Wahariri Tanzania TEF), wanashiriki kampeni ya kuboresha sheria nne zinazosimamia habari.

Sheria hizo ni Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016, Sheria ya Udhibiti wa Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010 (EPOCA), Sheria ya Haki ya Kupata Habari ya mwaka 2016 na Sheria ya Makosa ya Mitandaoni ya mwaka 2016 pamoja na kanuni za makosa ya mitandaoni za mwaka 2018 zilivyogawanya katika vipengele mbalimbali.

Mwenyekiti wa TEF, Deudatus Balile, akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu kampeni hiyo, alisema ina lengo la kufanya maboresho ya sheria hiyo.

Alisema kifungu cha tano cha Sheria ya Habari ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 kina vifungu viwili vyenye ukakasi.

"Kuna kifungu cha 5 (l) na 5 (e) ambacho kinampa mamlaka Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo kusajili magazeti. Hapa tumeona tatizo kubwa katika kusajili magazeti tumeona mwaka 2014, 2015 na 2016 wakati sheria hii ikiwa kwenye mchakato wa kupitisha kuwa kifungu hiki kina nia ovu hatukueleweka," alisema Balile.

Alisema madhara waliyaona ni kufungiwa magazeti ya Mwanahalisi, Mawio, Tanzania Daima na Mseto na kunyang'anywa leseni yasifanye biashara.

"Hapa tunasema kwamba kifungu hiki kifutwe, kirejeshwe kama zamani kuwa mtu akisajili gazeti linakuwa la kudumu isipokuwa asipochapisha ndani ya miaka mitatu ndipo leseni ilikuwa inajifuta," alisema.

Alisema kuvifungia vyombo vya habari ni kuathiri mawasiliano kati ya msomaji na chombo kilichofungiwa na wafanyakazi kupoteza ajira.

Balile alisema pia vyombo vinavyofungiwa vinakuwa na mikataba ambayo inaendelea na watangazaji hali inayosababisha hasara kubwa zaidi.

Alisema kifungu cha 5(l) kinampa mamlaka Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo kuchakata, kuruhusu kutangaza matangazo yote ya serikali na taasisi zake na chombo cha habari anachotaka hali ambayo inaweza kuleta urasimu au mazingira ya rushwa.

"Kama ambavyo alielekeza Rais Samia Suluhu Hassan Juni 26, mwaka jana, vyombo vya habari vipewe matangazo kwa njia ya ushindani na siyo kwa upendeleo au njia zinazoleta mashaka," alisisitiza.

Kadhalika alimshukuru Waziri Habari na Teknolojia ya Mawasiliano, Nape Nnauye kwa kuahidi kusimamia mchakato huo hadi kupata sheria yenye usawa kwa watendaji na serikali kwa ujumla.



Mhandisi wa Ujenzi wa Chuo Kikuu Ardhi (ARU), Twimanye John (kulia), akionyesha teknolojia rahisi ya kutengeneza tofali kwenye maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ARU yabuni teknolojia ya ujenzi rafiki kwa mazingira

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO Kikuu Ardhi (ARU), kupitia taasisi yake ya utafiti ya nyumba, imebuni teknolojia ya ujenzi wa gharama nafuu kwa kutumia matofali ambayo ni rafiki kwa mazingira.

Hayo yalibainika jana wakati wa maonyesho ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yanayoendelea kwenye viwanja vya Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete mkoani Dodoma.

Akizungumza kuhusu teknologia hiyo jana, Mhadhiri wa ARU, Dk. Given Mhina, alisema matumzi ya matofali ya aina hiyo zitasaidia kupunguza hewa ya ukaa duniani, kutunza na kuhifadhi mazingira.

Matofali hayo, alisema hutengenezwa kwa kutumia udongo wa mfinyanzi, saruji na maji kidogo na ni imara kwa matumizi mbalimbali ya shughuli za ujenzi.

"Tumekuja na teknojia hii kama sehemu ya jitihada ya kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa unaotokana na shughuli za ujenzi na mali ghafi zake kama vile saruji, mchanga na maji.... tunatumia udongo wa mfinyanzi na wakati mwingine vumbi linalotokana na utengenezaji wa kokoto," alisema.

Alisema ujenzi wa nyumba kwa kutumia tofali hizo hauhitaji saruji, mchanga wala maji kwani zinafungamana zenyewe isipokuwa wakati wa kuweka nguzo za nyumba pekee.

Dk. Mhina alisema hata wakati wa umaliziaji wa nyumba mtu aliyetumia tofali hizo halazimiki plasta ya saruji na mchanga badala yake mafundi watatumia mchanga na saruji kidogo sana kuziba mashimo na kisha mwonekano wa nyumba kuwa wa kuvutia.

Mtaalamu huyo alisema faida nyingine ya matumizi ya matofali ya aina hiyo ni kutosababisha joto ndani ya nyumba kulinganisha na matofali mengine yaliyozoeleka kwenye shughuli za ujenzi.

"Matofali yanayotengenezwa kwa kutumia saruji na mchanga yana tabia ya kufyonza joto wakati wa mchana na joto hilo kutoka wakati wa usiku lakini mfinyanzi unaotumika kutengeneza matofali haya unasababisha ubaridi kwasababu hauna tabia ya kufyonza joto," alisema.

"Ndiyo sababu kwenye chungu kilichotengenezwa kwa mfinyanzi ukiweka maji hata mchana wakati wa joto kali baada ya muda maji yanapata ubaridi na watu wengi wamekuwa wakitumia vyungu vya mfinyanzi kupata maji baridi," alisema.

Dk. Mhina ali kusema kuwa Taasisi ya Utafiti wa Nyumba ya ARU imekuwa ikifanya utafiti kwa vifaa vya ujenzi vinavyopatikana hapa nchini na kwingineko duniani.

Aliseama jukumu lingine la taasisi hiyo ni kuhakikisha matokeo ya tafiti wanazofanya zinawafikia walengwa kukuza na kuendeleza matumizi ya vifaa bora vya unjenzi nchini.

# NEMC yataja hatari tano vyanzo vya maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BARAZA la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC) limetaja sababu tano zinazochangia uharibifu wa vyanzo vya maji na maeneo oevu nchini.

Sababu hizo ni pamoja na ukaguzi wa NEMC kuonyesha mabadiliko ya matumizi ya ardhi kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo uanzishwaji wa miradi kufanyika bila kuangalia tathmini ya athari kwa mazingira.

Kutokana na hali hiyo, NEMC imewataka maofisa mazingira nchini kusimamia ipasavyo Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 sambamba na kutunga sheria ndogo za kulinda maeneo hayo.

Meneja wa NEMC Kanda ya Kati, Dk. Franklin Rwezimula, alibainisha hayo jana jijini hapa kwenye warsha ya maofisa mazingira wa mikoa na wilaya nchini alipowasilisha mada kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira kwenye maeneo hayo.

Alitaja sababu zingine ni wenye miradi kutokuzingatia mipango ya ufuatiliaji na usimamizi wa mazingira na athari nyingine za kimazingira katika migodi kutozingatia mpango wa uthibiti wa mazingira.

"Vilevile, mipango mingi inaanzishwa pasipo kupitia mchakato muhimu wa tathmini za kimkakati ya mazingira kwenye mipango hiyo kama ilivyoainishwa kwenye kifungu namba 104 cha Sheria ya Mazingira, pia baadhi ya wawekezaji kukiuka taratibu zilizopo kama zilivyoainishwa kwenye sheria," alisema.

Kiongozi huyo alisema maeneo mengi ya vyanzo vya maji nchini yamekumbwa na tatizo la uvamizi wa wafugaji na wakulima wakitafuta maji kwa ajili ya kunywesha mifugo na kilimo.

"Hali hii imesababisha vyanzo vingi vya maji kuharibiwa na kuchafuliwa na kupelekea uhaba wa maji katika baadhi ya maeneo nchini, vyanzo vya maji ni rasilimali muhimu inayochangia maendeleo ya nchi," alisema.

Meneja huyo alisema NEMC pamoja na maofisa hao wamejipanga kwenye utekelezaji wa majukumu yao kusimamia Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021.

"Suala la kudhibiti uharibifu wa mazingira kwenye vyanzo vya maji ni utekelezaji wa Sera ya Mazingira lakini ni utekelezaji wa maagizo aliyotoa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango alipokuwa akizindua sera ya mazingira mwaka huu, tumejiandaa kuwapitisha ninyi washiriki kwenye masuala mbalimbali," alisema.

Ili kuhakikisha ulinzi madhubuti wa vyanzo vya maji, meneja huyo alizisisitiza kamati za ulinzi na usalama za mikoa na wilaya kushiriki kikamilifu kwa kushirikiana na ofisi za mabonde ya maji katika kulinda vyanzo vya maji.

"Hii itahusisha vyombo vya dola kufanya operesheni za kushtukiza mara kwa mara kwani hii itasaidia kupunguza ama kuondokana na uchafuzi wa mazingira unaofanywa na watu kwenye nyanzo vya maji," alisema.

Mmoja wa maofisa hao, Ofisa Mazingira kutoka Wilaya ya Kakonko mkoani Kigoma, Bakari Bakari, alisema wapo tayari kuhakikisha mazingira na vyanzo vya maji vinatunzwa kwa kusimamia sheria, kanuni na taratibu za nchi.





## Mwalimu mstaafu afikishwa kortini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Kondoa imewafikisha mahakamani watuhumiwa wanne akiwamo mwalimu mkuu mstaafu wa Shule ya Msingi Hachwi kwa tuhuma za ubadhirifu na ufujaji wa mali ya umma.

Watuhumiwa hao walifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kondoa mbele ya Hakimu Mwajuma Lukindo na kusomewa shtaka hilo.

Washtakiwa hao ni Mwalimu Mkuu mstaafu Ramadhan Ramadhan (60), Solomon Mwankunga (37) ambaye ni mwalimu wa shule hiyo, Salimu Bura ambaye ni mwenyekiti wa bodi ya ununuzi ya shule na mfanyabiashara Bakari Abdalah.

Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU, Leonard Haule, alidai kuwa watuhumiwa hao wanakabiliwa na kesi ya uhujumi uchumi namba 3/2022.

Alidai kuwa watuhumiwa hao wametenda kosa hilo kinyume na kifungu cha Sheria Namba 28 za Kuzuia na Kupambana na Rushwa cha mwaka 2007.

Haule alidai kuwa watuhumiwa hao walitenda kosa hilo kati ya Juni 10 na Julai 20, 2018 na TAKUKURU ilifanya uchunguzi na kubaini ubadhirifu huo kwa watuhumiwa kuchepusha matofali 1,000 yenye thamani ya Sh. milioni 1.5 na kuisababishia serikali hasara.

Alidai kuwa washtakiwa hao baada ya kusomewa shtaka, walikana na kuachiwa kwa dhamana. Kesi hiyo itatajwa tena Juni 7, mwaka huu.

**Washtakiwa hao ni Mwalimu Mkuu mstaafu Ramadhan Ramadhan (60), Solomon Mwankunga (37) ambaye ni mwalimu wa shule hiyo, Salimu Bura ambaye ni mwenyekiti wa bodi ya ununuzi ya shule na mfanyabiashara Bakari Abdalah.**

# Waziri ahimiza utunzaji vyanzo maji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Maji, Maryprica Mahundi, amewataka Watanzania kutunza vyanzo vya maji ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa maji kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Mahundi alisema hayo jana alipokuwa akitoa tamko la Wizara ya Maji kuhusu ushiriki wake katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.

"Kutunza mazingira pamoja na rasilimali zinazozunguka kama rasilimali maji ni jukumu letu sote kwa kuwa Tanzania ni moja tu hakuna mbadala wa Tanzania.

"Kama mnavyofahamu maji ni moja ya rasilimali adhimu, maji ni uhai, maji hayana mbadala, hivyo kaulimbiu ya mwaka huu inahimiza kutunza vema rasilimali tuliyo nayo ili kulinda Tanzania yetu," alisema. Mahundi alisema hifadhi ya vyanzo vya maji ni muhimu ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa huduma hiyo kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

"Kaulimbiu inakwenda sambamba na tamko la Rais Samia Suluhu Hassan alilotoa tarehe 22 Machi 2022 jijini Dar es Saalam, wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Maji kwamba Watanzania kutunza mazingira hususani uoto wa asili kwa kuepuka kukata au kuchoma miti ovyo," alisema.

Alisema katika maeneo ya vijijini chemchemu nyingi za maji pamoja na baadhi ya mito imetoweka kutokana na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli za kibinadamu karibu na vyanzo vya maji.

"Kama inavyosema kaulimbiu ya mwaka huu Tanzania ni moja tu, tutunze mazingira, vyanzo vya maji vikikauka vitahatarisha hata uwapo wa maji Tanzania, hivyo uhai wetu utakuwa hatarini, ndiyo maana tunasema maji ni uhai. Maji hayana mbadala, unaweza ukakosa nishati ya umeme wa maji ukatumia nishati mbadala kama jua na gesi lakini bila maji hakuna uhai," alisema.

Kadhalika, alisema ili kuhimiza umuhimu wa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani wizara imetoa maelekezo kwa taasisi zake zote kushiriki ipasavyo katika maadhimisho hayo katika ngazi ya mkoa na wilaya.

"Aidha kwa kuwa maadhimisho ya kitaifa yanafanyika jijini Dodoma yakiambatana na maonyesho katika viwanja vya nje ya ukumbi wa Jakaya Kikwete, wizara na taasisi zake zinashiriki katika maonyesho hayo.

"Hivyo nitumie fursa hii kuwakaribisha wananchi wote kutembelea mabanda ya taasisi zetu ili kupata ufafanuzi wa huduma zinazotolewa na wizara," alisema.

Hata hivyo, alitoa maelekezo kwa taasisi zote kushirikiana na wadau mbalimbali katika kusimamia utunzaji wa rasilimali za maji.

"Kumekuwa na mtazamo wa kwamba Bodi za Maji pekee ndizo zenye jukumu la kusimamia na kutunza vyanzo vya maji tutambue kwamba kutunza vyanzo vya maji ni jukumu letu sote," alisisitiza Mahundi.



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dk. John Jingu (katikati), akiongoza kikao cha Kamati Tendaji ya Kitaifa ya Uratibu wa Operesheni Anwani za Makazi, jijini Dodoma, jana. Kulia ni Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kaspar Mmuya na Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Clarence Ichwekeleza. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Wakutana kujadili rasimu ya mkataba

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WADAU wa mifugo na uvuvi wamekutana jijini Dodoma kutoa maoni kuhusu rasimu ya mkataba wa huduma kwa wateja huku wakipendekeza mambo mbalimbali.

Akizungumza jana wakati wa mkutano wa wadau wa kutoa maoni kuhusu rasimu ya mkataba wa huduma kwa wateja, Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Charles Mhina, alisema mkataba huo ni muhimu kwakuwa unawasaidia kwenye kujiendesha kiweledi.

"Uadilifu weledi na uwajibikaji tunatakiwa kwenda katika misingi ambayo inazingatia kanuni za utumishi wa uuma. Kwenye eneo la weledi ni lazima kuwe na viwango vya huduma bora kama taasisi ndipo pale tunapopambanua kuwafikia wateja wetu kila kundi lina matarajio yake," alisema.

"Ukiwa shambani kwako tunakuhudumia kwa huduma za ugani tunahakikisha tunakufikishia kwa wakati na kwenye mifugo hivyo hivyo. Hata kwenye masoko tunafanya hivyo hivyo pamoja na huduma za vibali haya yote yanagusa katika weledi.

Alisema wana matarajio makubwa watafikia malengo ya kutoa huduma bora ambazo zitaleta mabadiliko makubwa.

"Ninaamini tutafikia viwango na huduma zitaweza kuwafikia watu wengi tunafanya mapitio ya mkataba ulioandaliwa tangu mwaka 2014 hivyo kuna mabadiliko mengi ambayo yametokea. Kuna mabadiliko ya kiteknolojia tulikuwa katika analogy lakini sasa hivi tunatoa vibali kwa kutumia TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano)," alisema.

Ofisa Tawala Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wamoja Ayubu, ambaye ni mratibu wa rasimu ya mkataba kwa mteja, alisema mkataba huo unaelezea namna ambavyo mteja anaweza kurejesha mrejesho wa huduma ambayo amepata.

"Mchakato huu ulianza tangu Machi. Katibu Mkuu aliunda timu ambayo ilikaa na kupitia na tulitoka na rasimu na Mei iliwasilishwa kwenye wizara na mapendekezo yalitolewa sasa rasimu tumekuja kuwasilisha kwa wadau," alisema.

Alisema mkataba huo ni muhimu kwani unapima utendaji wa taasisi ambapo wateja wataweza kuwapima kama wanafikia vile viwango.

Naye, Ofisa Uhusiano na Masoko kutoka Kampuni ya Kilimanjaro International Leather Industries (KLIC), Fredrick Njoka, alisema wamehudhuria mkutano huo kama wanufaikaji na wanataka kuhakikisha wizara inakuwa na mikakati ambayo inawanufaisha wao.

"Zile changamoto ambazo tulikuwa tunaziona tunazitoa hapa hili ni jambo shirikishi na muhimu na hii ndio sehemu pekee ya kuelezea kuna vitu vingi ambavyo tunataka viongezeke," alisema.



# SMZ yaelekeza nguvu katika kilimo cha mwani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SAFARI ya kuelekea katika uchumi wa buluu imeanza rasmi na kwamba kilimo cha mwani kinacholimwa na wakulima asilimia 95 ya wanawake kimepewa kipaumbele cha kwanza ili kuwa mkombozi katika kuinua hali za maisha yao, imeelezwa .

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Suleiman Masoud Makame, wakati akijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Waziri Makame alisema kilimo cha mwani ni miongoni mwa vipaumbele katika makadirio ya wizara hiyo na kwamba kimetajwa katika ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 huku ikilenga katika kuwakomboa wakulima ambao kwa asilimia 90 ni wanawake walioko vijijini.

Aliitaja mikakati iliyochukuliwa na wizara hiyo katika bajeti ya mwaka 2022/23 kuwa ni pamoja na kujenga kiwanda cha kusarifu na kuongeza thamani ya uzalishaji wa mwani kwa ajili ya kupata faida kubwa kwa wakulima.

"Kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kusarifu na kuongeza thamani ya uzalishaji wa mwani kwa ajili ya matumizi mbalimbali hatua ambayo italeta tija kubwa kwa wakulima wake," alisema.

Pia alisema serikali inatarajia kujenga kiwanda cha kusarifu na kuongeza thamani ya mwani Chamanangwe mkoa wa Kaskazini Pemba na kununua boti 500 ambazo zitatumiwa na wakulima kuwawezesha kufika katika kina kikubwa cha maji baharini.

Alisema kutokana na kuwapo kwa mabadiliko makubwa ya kilimo hicho ambacho kimekabiliwa na mabadiliko ya tabia ya nchi, hivi sasa kinalimwa katika kina kikubwa, hivyo wakulima wanahitaji kupata vifaa vya kufika maeneo hayo ambayo ni boti.

Waziri alibainisha kuwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imetenga Sh. bilioni 10 ambazo zitatumika kwa ajili ya kuwawezesha wakulima wa mazao ya baharini yakiwamo mwani, majongoo bahari na ufugaji wa samaki na kaa.




Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Suleiman Masoud, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMA**

## Watumishi ZEC wapewa mafunzo

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Uchaguzi wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Khamis Kona Khamis, amewataka watendaji wa tume hiyo kujenga tabia ya kuzisoma mara kwa mara sheria na kanuni za uchaguzi kwa lengo la kuimarisha weledi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Khamis aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo watendaji wa tume hiyo yaliofanyika katika ofisi za ZEC, mjini Unguja.

Alisema inapendeza mtumishi wa umma kuzijua sheria, kanuni, sera na miongozo ambayo inasimamiwa na taasisi kulingana na majukumu yake ili kumfanya ajiamini katika utekelezaji.

Mkurugenzi huyo alisema afisi ya tume imejiwekea mkakati wa mafunzo elekezi kwa watendaji wake ili kumwezesha kila mmoja kuyajua majukumu yote ya tume ambayo yameelezwa katika sheria za uchaguzi pamoja na aheria zingine ikiwamo sheria ya kuanzishwa ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar Na. 1 ya mwaka 2017.

Akiwasilisha mada kuhusu mzunguko wa mchaguzi, Mkurugenzi wa Mipango, Utumishi na Utawala, Saadun Ahmed Khamis, alisema uchaguzi ni mchakato ambao unajumuisha matukio mengi ndani ya kipindi cha miaka mitano nchini, hivyo kumalizika kwa uchaguzi mmoja huwafanya watendaji wa tume kuingia katika awamu ya mzunguko wa uchaguzi mwingine.

Saaduni alisema mzunguko wa uchaguzi unatofautiana kwa mujibu wa katiba za nchi na kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, mzunguko wa uchaguzi nchini Tanzania ni mchakato wa miaka mitano ambao hujumuisha awamu tatu za mzunguko huo yaani kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Uchaguzi, Khamis Issa Khamis na Mkurugenzi wa Huduma za Sheria, Maulid Ame Muhammed, walisema uchaguzi ni mchakato unaoendeshwa kwa mujibu wa sheria, hivyo ni vyema kila mdau wa uchaguzi kuvijua vifungu vyote vya sheria ili kuendana na misingi ya uendeshaji wa uchaguzi.

# SMZ yajipanga kukabiliana na athari mabadiliko ya tabianchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema itaendelea kuchukua juhudi za kukabiliana na athari za mazingira ambazo kwa kiasi kikubwa zimechangiwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mabadiliko hayo yamesababisha athari mbalimbali duniani huku maeneo mengi ya visiwa vidogo yakiwa katika tishio la kutoweka.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, alisema hayo jana wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambayo kwa Zanzibar yatafanyika kwa kufanya usafi katika maeneo ya fukwe na kuotesha mikoko pembezoni mwa fukwe za bahari.

Alisema Zanzibar haiko salama na athari za mazingira zinazotokana na kasi ya mabadiliko ya tabia nchi ambayo kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na shughuli za kibinadamu.

Kwa mujibu wa waziri, ukubwa wa visiwa vya Unguja na Pemba umeanza kupungua kutokana na kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya makazi na kusababisha tishio kwa maisha ya binadamu.

Alizitaja juhudi zinazochukuliwa na serikali kwa kuwashirikisha washirika wa maendeleo kuwa ni pamoja na kuotesha miti inayozuia kasi ya maji kuvamia maeneo ya fukwe ikiwamo mikoko.

"Tumeanza kuwashajihisha wananchi wetu kuotesha mikoko kwa wingi pembezoni mwa bahari kwa ajili ya kuzuia kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya fukwe," alisema.

Waziri pia alikemea tabia iliyojitokeza kwa baadhi ya wananchi kuchota mchanga wa baharini ambao ni tishio na kusababisha kasi ya maji kuja juu.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA


# WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII, MHE. BALOZI DKT, PINDI HAZARA CHANA (Mb), WAKATI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/23






MHE. BALOZI DKT, PINDI HAZARA CHANA (Mb)
WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII



DKT. FRANCIS KASABUBU MICHAEL
KATIBU MKUU WA MALIASILI NA UTALII



MHE. MARY FRANCIS MASANJA (Mb)
NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII



BW. JUMA SELEMANI MKOMI
NAIBU KATIBU MKUU WA MALIASILI NA UTALII

# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII MHESHIMIWA BALOZI DKT. PINDI H. CHANA (MB.) WAKATI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**1.0 UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha, ninaomba Bunge lako lijadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuendelea kujenga uchumi na maendeleo ya nchi yetu. Aidha, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa dhati kabisa, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kunipa dhamana ya kusimamia Wizara hii yenye umuhimu mkubwa kwa Taifa na jamii kwa ujumla. Ninaomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu kumuombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kumpa nguvu na afya njema ili aendelee kuwatumikia Watanzania.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Philip Isdori Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao thabiti katika kusimamia maliasili, malikale na kuendeleza utalii. Kupitia miongozo na maelekezo yao mazuri na yenye tija, Wizara imeendelea kutimiza wajibu wake kwa kuimarisha uhifadhi na kuendeleza utalii na hivyo kuchangia katika juhudi za kukuza uchumi na ustawi wa wananchi kwa ujumla. Aidha, nikupongeze wewe binafsi, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), Spika wa Bunge na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuliongoza Bunge letu Tukufu. Imani hiyo imejengeka kutokana na umahiri na weledi mkubwa mliouonesha katika kuliongoza Bunge hili. Vilevile, niwapongeze Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha shughuli za Bunge letu kwa weledi mkubwa.

4. **Mheshimiwa Spika**, kwa dhati, ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Ally Juma Makoa (Mb.), Mbunge wa Kondoa Mjini kwa kujadili, kushauri na kupitisha mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa namna ya kipekee, niseme kwa uwazi kuwa Kamati hii imekuwa na mchango mkubwa katika kuishauri Wizara kupitia maoni na maelekezo yake. Wizara itaendelea kuzingatia maoni na ushauri wa Kamati na Bunge lako Tukufu ili kufanikisha malengo yake.

5. **Mheshimiwa Spika,** naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionitangulia kumpongeza Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninaomba nitumie fursa hii adhimu kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa juhudi kubwa wanazozifanya katika kusimamia na kuhifadhi maliasili; na kuendeleza utalii. Vilevile, ninawashukuru wananchi wa Mkoa wa Njombe kwa kuendelea kuniunga mkono kwa dhati katika kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge na Waziri wa Maliasili na Utalii. Ninapenda kuwahimiza wote kushiriki katika uhifadhi wa maliasili, malikale na kuendeleza utalii kwa maendeleo endelevu ya nchi yetu.

6. **Mheshimiwa Spika,** ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi wenzangu wa Wizara akiwemo Mheshimiwa Mary Francis Masanja (Mb.), Naibu Waziri; Dkt. Francis Kasabubu Michael, Katibu Mkuu; na Ndugu Juma Selemani Mkomi, Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, nimpongeze mtangulizi wangu Mheshimwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb.), Waziri wa Katiba na Sheria kwa mchango wake alioutoa katika kufanikisha majukumu mbalimbali ya Wizara. Vilevile, ninawashukuru Watendaji Wakuu na Watumishi wa Wizara; na wadau wote wa Sekta ya Maliasili na Utalii kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia katika kuiongoza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa.

7. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi wote wa Serikali wakiwemo waheshimiwa mawaziri, wabunge na wakuu wa taasisi; pamoja na watumishi, ndugu, jamaa na marafiki kwa jinsi walivyojitoa katika kutufariji na kufanikisha mazishi ya marehemu mama yetu mpendwa Regina Mlowe. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

8. **Mheshimiwa Spika,** nitumie nafasi hii kutoa pole kwako, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na watanzania wenzangu kwa kuondokewa na wapendwa wetu: Mheshimiwa Elias Kwandikwa, aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu; Mheshimiwa William Tate Olenasha aliyekuwa Naibu Waziri wa Uwekezaji (Ofisi ya Waziri Mkuu) na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro; Mheshimiwa Khatibu Said Haji aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde Zanzibar; na Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa. Aidha, natoa pole kwa ndugu, marafiki na watumishi wote wa Wizara kutokana na watumishi 10 waliopoteza maisha wakati wakitekeleza majukumu yao. Kwa hakika, watumishi hawa ni mashujaa ambao wamepoteza maisha wakitetea rasilimali za nchi yetu. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina. Pia, nitumie fursa hii kutoa pole kwa watumishi waliojeruhiwa wakati wanatekeleza majukumu yao. Sambamba na hilo, ninatoa pole za dhati kwa wananchi ambao wamepata madhara kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu na hivyo kujeruhiwa, kupoteza ndugu na kuharibiwa mali zao.

9. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba sasa kuwasilisha hotuba yangu ambayo imejikita katika Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**2.0 MCHANGO WA MALIASILI NA UTALII KATIKA KUKUZA UCHUMI NA MAENDELEO ENDELEVU**

10. **Mheshimiwa Spika,** Tanzania imebarikiwa kuwa na rasilimali za maliasili na malikale zenye mchango mkubwa katika uendelezaji utalii, ustawi wa wananchi na ukuaji wa uchumi. Aidha, maeneo ya hifadhi ndiyo vyanzo vikuu vya maji, nishati, makazi ya wanyamapori na viumbe wengine, uhifadhi wa udongo na ufyonzaji wa hewa ukaa, hali inayopunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Vilevile, malikale zinatumika kuhifadhi historia na tamaduni zetu. Hivyo, ninaomba nitumie fursa hii kutoa rai kwa Watanzania wote na wadau wa sekta ya maliasili na utalii nchini, kuendelea kushirikiana na Wizara kuhifadhi maliasili, malikale na kuendeleza utalii, kwa maendeleo ya Taifa letu na dunia kwa ujumla.

**3.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/2022**

**3.1 UKUSANYAJI MADUHULI**

11. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya Shilingi bilioni 689.35. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 478.01 zinakusanywa na Wizara kupitia mfumo wa TRA kutoka vyanzo vya TANAPA, NCAA na TAWA na Shilingi bilioni 211.33 zinakusanywa moja kwa moja na Wizara kupitia mfumo wa MNRT Portal kutoka Idara, mifuko na taasisi nyingine za Wizara. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Wizara imekusanya jumla ya Shilingi bilioni 396.27 sawa na asilimia 57 ya lengo la makusanyo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 249.83 zimekusanywa kupitia TRA na Shilingi bilioni 146.44 zimekusanywa na Wizara.

**3.2 MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO**

12. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya Shilingi bilioni 571.63 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya Fedha hizo, Shilingi bilioni 418.86 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 152.77 ni miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Wizara na Taasisi zake ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi bilioni 474.35 sawa na asilimia 83 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 357.75 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 116.61 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**3.3 MAFANIKIO**

13. **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara imepata mafanikio mbalimbali yakiwemo:

(i) Utangazaji Utalii na Kuvutia Uwekezaji kupitia Programu Maalum ya Tanzania - The Royal Tour

14. **Mheshimiwa Spika,** kipekee kabisa, napenda kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudi zake kubwa za kuitangaza nchi yetu kimataifa kupitia programu ya Tanzania – The Royal Tour. Programu hiyo imewezesha kuitambulisha Tanzania kimataifa kwa kutangaza vivutio vya utalii vya kipekee vya nchi yetu; kuonesha fursa mbalimbali za uwekezaji kwenye sekta ya maliasili na utalii pamoja na kuimarisha nafasi ya nchi katika jumuiya za kimataifa. Programu hii ilizinduliwa mwezi Aprili, 2022 katika Jiji la New York na Jiji la Los Angeles nchini Marekani; na kuendelea katika Jiji la Arusha, Dar es Salaam, Zanzibar na Dodoma. Katika uzinduzi nchini Marekani, zaidi ya watu 6,000 walishiriki wakiwemo viongozi wa kitaifa; viongozi wa majiji husika; watu maarufu; wawekezaji; wadau wa utalii na uhifadhi; na wafanyabiashara mbalimbali. Uzinduzi huo pia ulishirikisha vyombo mbalimbali vya habari vya kimataifa vikiwemo: vituo vya televisheni na redio vya CBS, Fox News, NBC, YouTube na PBS - Amazon Prime video.

15. **Mheshimiwa Spika,** programu ya Tanzania – the Royal Tour imeanza kuleta matunda kwa kuvutia watalii na wawekezaji mbalimbali kutembelea nchini. Mathalan, wakala wa utalii zaidi ya 30 kutoka katika masoko ya utalii yakiwemo Marekani, Ufaransa na Lithuania wamehamasika kutembelea nchini ili kujifunza na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii kwa lengo la kuvitangaza katika nchi zao. Aidha, wawekezaji kutoka Taifa la Bulgaria wameonesha nia ya kuwekeza nchini kwa kujenga hoteli nne (4) zenye hadhi ya nyota tano (5) katika hifadhi za Taifa Serengeti, Ziwa Manyara na Tarangire; na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. katika hatua nyingine, Serikali imesaini mkataba wa ushirikiano katika masuala ya utalii, biashara na uwekezaji baina ya Tanzania na Jiji la Dallas Marekani. Hatua hiyo itafungua fursa za usafiri wa anga kwa kuwezesha safari za moja kwa moja za ndege kutoka Tanzania hadi Dallas, Marekani na hivyo kuongeza idadi ya wageni nchini.

16. **Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kuendelea kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kutangaza utalii na kuvutia uwekezaji kwa maslahi mapana ya Taifa na ustawi wa jamii kwa ujumla.

(ii) Tanzania kuendelea Kutambulika Kimataifa katika Masuala ya Utalii na Uhifadhi

17. **Mheshimiwa Spika,** Tanzania imeendelea kutambulika kimataifa na kupata tuzo mbalimbali zikiwemo: Hifadhi ya Taifa Serengeti kuwa hifadhi inayoongoza kwa ubora Barani Afrika kwa miaka mitatu (3) mfululizo kuanzia mwaka 2019 hadi 2021; na Tanzania kuwa nchi inayoongoza kwa shughuli za utalii Barani Afrika. Tuzo hizi zilitolewa na World Travel Award. Tuzo nyingine ni pamoja na Travellers' Choice Destination – National Parks of the World, iliyotolewa na Tripadvisor ambapo Tanzania imeingiza hifadhi nne (4) katika orodha ya hifadhi 25 bora duniani zikiongozwa na Hifadhi ya Taifa Serengeti. Hifadhi nyingine ni Hifadhi za Taifa Kilimanjaro na Tarangire; na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Aidha, Zanzibar na Jiji la Arusha zimeorodheshwa na Tripadvisor kupitia Travellers' Choice Destination – Afrika kuwa miongoni mwa maeneo 10 bora ya shughuli za utalii Barani Afrika.

(iii) Kuongezeka kwa Malighafi ya Mazao ya Misitu kwa ajili ya Viwanda

18. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuongeza upatikanaji wa malighafi ya mazao ya misitu katika mashamba ya miti ya Serikali kutoka mita za ujazo 729,000 kwa mwaka 2020/2021 hadi wastani wa mita za ujazo 1,000,000 kwa mwaka 2021/2022. Mafanikio haya yametokana na juhudi mbalimbali zikiwemo: kuendeleza mashamba ya miti kwa kupanda miche zaidi ya milioni 29; na kuanzisha Shamba jipya la Miti la Makere, Mkoa wa Kigoma lenye ukubwa wa hekta 29,827.

(iv) Kuongezeka kwa Matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki katika Uendeshaji wa Minada ya Mazao

# HOTUBA

ya Misitu na Wanyamapori

19. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeongeza matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kuendesha minada ya mazao ya misitu na wanyamapori. Mathalan, Wizara imefanikiwa kuendesha jumla ya minada saba (7) ya kielektroniki iliyojumuisha vitalu 100 vya uwindaji wa kitalii. Kati ya vitalu hivyo, 64 vimeuzwa na kufanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 18.1 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi bilioni 5.0 ambacho kingekusanywa kwa njia ya kiutawala (administrative allocation).

(v) Kuendeleza Utalii Ikolojia katika Hifadhi za Misitu za Mazingira Asilia

20. **Mheshimiwa Spika,** katika kupanua wigo wa mazao ya utalii nchini, Wizara imeendelea kuboresha miundombinu ya utalii ikolojia katika hifadhi za misitu ya mazingira asilia zikiwemo hifadhi za Amani, Pugu Kazimzumbwi, Magamba na Ziwa Duluti. Baadhi ya juhudi zilizofanyika ni ukarabati wa barabara zenye urefu wa kilomita 66.7, njia za watembea kwa miguu kilomita 163.2 na ujenzi wa kambi tano (5) za kitalii.

(vi) Sekta ya Utalii Kuendelea kuwa Stahimilivu (Resilient) katika kipindi cha UVIKO-19

21. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na changamoto ya uwepo wa janga la UVIKO-19, sekta ya utalii nchini imeendelea kuwa stahimilivu ambapo idadi ya watalii na mapato yameendelea kuongezeka. Mathalan, katika mwaka 2021, Tanzania imefanikiwa kupokea jumla ya watalii wa kimataifa 922,692 ikiwa ni ongezeko la asilimia 48.6 kutoka watalii 620,867 kwa mwaka 2020. Aidha, mapato yatokanayo na watalii wa kimataifa yameongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 714.59 mwaka 2020 hadi Dola za Marekani bilioni 1.3 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 83. Mafanikio hayo yamechochewa na juhudi mbalimbali zilizofanywa na Wizara.

(vii) Kukua kwa Utalii wa Ndani

22. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhamasisha utalii wa ndani kupitia kampeni na programu mbalimbali. Hatua hizi zimeongeza idadi ya watalii wa ndani waliotembelea maeneo ya hifadhi, vituo vya malikale na makumbusho kutoka watalii 562,549 mwaka 2020 hadi 788,933 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 40.2. Ongezeko la idadi ya watalii limechangiwa na juhudi mbalimbali zikiwemo: kampeni za kutangaza utalii, maadhimisho na maonesho mbalimbali.

(viii) Kupungua kwa Ujangili na Uvunaji Haramu wa Maliasili

23. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuongeza jitihada za kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa rasilimali za maliasili kwa kudhibiti ujangili, biashara haramu ya nyara, uvunaji haramu wa mazao ya misitu na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa. Jitihada hizo zinadhihirishwa na matokeo ya sensa ya wanyamapori iliyofanyika mwaka 2021 ambapo idadi ya tembo imeongezeka kwa asilimia 30 katika Mfumo Ikolojia Ziwa Natron - West Kilimanjaro. Aidha, katika Mfumo Ikolojia Ruaha – Rungwa, idadi ya nyati imeongezeka kwa asilimia 80; pundamilia asilimia 36; na palahala asilimia 65 ikilinganishwa na sensa iliyofanyika mwaka 2018. Pia, idadi ya faru weusi ambao wako hatarini kutoweka imeongezeka kwa asilimia 27.5 ikilinganishwa na idadi yao kwa mwaka 2018. Ongezeko la wanyamapori hao ni kiashiria cha kuimarika kwa ulinzi na usimamizi wa maeneo ya hifadhi.

(ix) Kuimarika kwa Utalii wa Urithi wa Utamaduni na Malikale

24. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea vituo vya malikale na makumbusho kutoka 349,264 mwaka wa fedha 2020/2021 hadi kufikia 582,080 mwezi Aprili, 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 167. Ongezeko hilo limechochewa na juhudi mbalimbali zikiwemo: kuanzisha programu maalum za kuhamasisha makundi katika jamii kutembelea vivutio vya malikale na makumbusho; kufanya matamasha ya utamaduni katika maeneo mbalimbali nchini; kuanzisha jarida maalum la makumbusho; kufanya mikutano maalum na wahariri wa vyombo vya habari; na kuimarisha miundombinu katika maeneo ya malikale na makumbusho.

**3.4 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA**

**3.4.1 SEKTA YA WANYAMAPORI**

25. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Wanyamapori ina jukumu la kuhifadhi, kusimamia, kutoa mafunzo na kufanya tafiti za wanyamapori ndani na nje ya maeneo ya hifadhi. Katika mwaka wa fedha 2021, Wizara imetekeleza shughuli mbalimali kama ifuatavyo:-

26. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa elimu ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa jamii zinazoishi karibu na maeneo ya hifadhi. Aidha, wizara imetumia teknolojia ya kufuatilia nyendo za wanyamapori hao kwa kuwafunga vifaa maalum vya kusukuma mawimbi ili kurahisisha ufuatiliaji. Katika kufanikisha zoezi hilo, jumla ya tembo 107; mbwa mwitu saba (7); faru 64; nyumbu 10; na simba 21 walifungwa mikanda ya mawasiliano (GPS collar) ili kuwezesha kufuatilia mienendo yao. Katika hatua nyingine, mwaka 2021/2022 Wizara imetenga fedha kiasi cha Shilingi 1,230,000,000 kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa vituo 11 vya askari wa kuzuia wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo korofi nchini. Tayari fedha hizo zimetolewa na Wizara ya Fedha na Mipango na sasa ujenzi unaendelea.

27. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha Kanuni na Amri za Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu. Aidha, imefanya mapitio ya Kanuni za Utalii wa Picha za mwaka 2016; Kanuni za Uwekezaji Mahiri ya mwaka 2021; Kanuni ya Mashamba ya Wanyamapori ya mwaka 2020; na Kanuni za Biashara ya Nyara ya mwaka 2010. Vilevile, taratibu za usajili wa magari ya Jeshi la Uhifadhi kutoka namba za kiraia kwenda namba za kijeshi zimekamilika ambapo magari 1,338 kati ya 1,699 yamepata usajili huo.

(i) Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania - TANAPA

28. **Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha mahusiano kati ya hifadhi na jamii Shirika limetoa elimu ya uhifadhi kwa vijiji 477 vinavyopakana na hifadhi za Taifa. Aidha, Shirika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali limetoa chanjo 63,005 dhidi ya ugonjwa wa mapafu kwa ng'ombe, kondoo na mbuzi katika vijiji 12 vinavyopakana na hifadhi za Taifa Mkomazi na Tarangire. Hatua hii inalenga kuzuia milipuko na kusambaa kwa magonjwa yanayoweza kuathiri wanyamapori. Katika hatua nyingine, Shirika limeendelea kuboresha miundombinu ya utalii kwa kujenga madaraja mawili (2) katika hifadhi ya Taifa Tarangire na Ruaha; kukarabati barabara zenye urefu wa kilomita 3,157 katika hifadhi 16 na kukarabati viwanja vya ndege 12 katika Hifadhi za Taifa za Ruaha, Serengeti, Nyerere, Tarangire, Saadani, Mikumi na Mkomazi.

29. **Mheshimiwa Spika,** Shirika limejenga "cottages" 13 zenye jumla ya vitanda 79 katika hifadhi za Taifa ili kuwezesha huduma ya malazi kwa watalii wa ndani na nje ya nchi. Aidha, Shirika limetoa maeneo 41 kwa wawekezaji kwa ajili ya kujenga miundombinu ya huduma za malazi kwa watalii yenye uwezo wa kubeba vitanda 2,250. Vilevile, jumla ya maeneo mapya 103 yenye uwezo wa vitanda 5,500 yameainishwa katika hifadhi za Taifa.

(ii) Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania - TAWA

30. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imetoa jumla ya leseni 36 za ufugaji wa wanyamapori kwa wawekezaji wa bustani, mashamba na ranchi za wanyamapori; na leseni 34 kwa ajili ya kuendesha biashara ya nyamapori. Aidha, Mamlaka imetoa maeneo saba (7) kwa wawekezaji chini ya utaratibu wa uwekezaji mahiri katika mapori ya akiba na tengefu. Uwekezaji huo umeiwezesha Mamlaka kuongeza mapato yatokanayo na shughuli za uwindaji wa kitalii kutoka Shilingi Bilioni 4.2 kwa mwaka 2021 hadi Shilingi Bilioni 22.1 mwezi Aprili, 2022 sawa na asilimia 426.2. Katika hatua nyingine, Mamlaka imefungua na kujenga barabara zenye urefu wa kilomita 321.5 kwa kiwango cha changarawe na madaraja mawili (2) katika mapori ya akiba 11. Aidha, Mamlaka imeanzisha ranchi sita (6); mashamba ya wanyamapori 27; na bustani za wanyamapori 24 ili kurahisisha upatikanaji wa nyamapori kwa wananchi.

(iii) Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro - NCAA

31. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imekarabati vituo sita (6) vya askari katika maeneo ya Lemala, Makhoromba, Ndutu, Kakesio, Endamagha na Masamburai; na ujenzi wa vituo vipya vya askari katika maeneo ya Lositete na Lemala unaendelea. Pia, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 4.2 inayoshuka kreta ya Ngorongoro kwa kiwango cha tabaka gumu la mawe. Sambamba na hilo, Mamlaka imekarabati barabara zenye urefu wa kilomita 472 ndani ya Hifadhi; na miundombinu ya viwanja vya ndege vya Ndutu na Ngorongoro. Aidha, Mamlaka imegawa mizinga 1,878 kwa vikundi 94 vya wafugaji nyuki katika wilaya za Ngorongoro, Karatu, Monduli na Meatu. Vilevile, Mamlaka imewezesha utoaji wa huduma za afya kwa wenyeji katika Zahanati ya Ngorongoro; kuwapatia wenyeji 1,300 kadi za bima ya afya ya jamii iliyoboreshwa (iCHF); na kutoa chanjo kwa jumla ya mifugo 2,040.

32. **Mheshimiwa Spika,** ili kutafuta suluhu ya kudumu ya changamoto za matumizi mseto ya ardhi ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mamlaka imefanya uhamasishaji kupitia vikao na mikutano ya majadiliano baina ya Serikali na wadau mbalimbali wakiwemo wenyeji waishio ndani ya eneo la Hifadhi. Kupitia jitihada hizo, jumla ya kaya 278 zenye wakazi 1,439 wamejiandikisha kuhama kwa hiari kutoka hifadhini. Pia, Wizara imebainisha maeneo mbadala yaliyopo Handeni, Tanga na Kitwai, Manyara kwa ajili ya makazi kwa wananchi watakaohama kutoka Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Kwa upande wa Handeni, Mamlaka imebainisha eneo lenye ukubwa wa hekta 112,239 kwa ajili ya matumizi ya makazi na huduma za jamii. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Wizara ilifanikiwa kupima eneo lenye ukubwa wa hekta 73,528.73 lililogawanywa kwa ajili ya matumizi mbalimbali yakiwemo: makazi (hekta 10,080.4), kilimo (hekta 13,628.48), malisho (hekta 22,176.06), ujenzi wa taasisi za elimu ya juu na vyuo (hekta 1,329.37), ushoroba wa wanyamapori (hekta 26,314.42) na hifadhi ya misitu (hekta 6,082.72). Zoezi la upimaji na upangaji wa matumizi ya ardhi katika eneo lililobaki pamoja na eneo la Kitwai lenye ukubwa wa hekta 409,416 linaendelea.

(iv) Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori - TAWIRI

33. **Mheshimiwa Spika,** Taasisi imeidadi wanyamapori katika mifumo ikolojia ya Ruaha – Rungwa na Katavi - Rukwa; maeneo ya mtawanyiko; na shoroba zilizomo katika mifumo ikolojia hiyo. Mathalan, Matokeo ya sensa katika mfumo ikolojia wa Ruaha - Rungwa yanaonesha kuwa kuna tembo 15,608, nyati 20,911, swala pala 8,643, pundamilia 10,552, palahala 6,636 na kongoni 4,017. Aidha, matokeo hayo yakilinganishwa na yale ya mwaka 2018 yanaonesha kuimarika kwa idadi ya tembo sambamba na ongezeko la nyati kwa asilimia 80, pundamilia asilimia 36, na palahala asilimia 65. Kwa ujumla, takwimu zinaonesha maoneo yaliyohifadhiwa yamezidi kuimarika. Vilevile, Taasisi ilitoa mafunzo ya mbinu za kukabiliana na migongano baina ya binadamu na wanyamapori kwa waelimishaji 610 katika wilaya 21 watakaotoa mafunzo kwa jamii kuhusu ya namna ya kukabiliana na wanayamapori wakali na waharibifu.

(v) Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - Mweka

34. **Mheshimiwa Spika,** Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 834 katika ngazi za Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 22 juu ya mbinu ya kukamata na kuhamisha nyoka katika eneo la Bulyankulu, Mkoa wa Shinyanga na mafunzo kwa waongoza watalii wapatao 1,060 kutoka katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Vilevile, Chuo kimejenga kumbi mbili (2) za mihadhara katika kampasi kuu ya Mweka na eneo la Mafunzo kwa Vitendo la Kwakuchinja lililopo wilayani Babati. Kumbi hizi zinauwezo wa kuchukua wanafunzi 250 kila moja. Pia, Chuo kimekamilisha ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 294 katika kampasi kuu ya Mweka.

(vi) Taasisi ya Taaluma ya Usimamizi wa Wanyamapori Pasiansi

35. **Mheshimiwa Spika,** Taasisi imedahili wanafunzi 410 katika fani za uhifadhi wanyamapori na himasheria, uongozaji watalii na usalama kwa ngazi ya Astashahada na Astashahada ya awali. Aidha, Taasisi imetoa mafunzo ya utayari wa Jeshi la Uhifadhi kwa watumishi wapya 43 wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania. Katika hatua nyingine, Taasisi imetoa mafunzo ya muda mfupi kuhusu usimamizi wa rasilimali za wanyamapori kwa jumla ya wanavijiji 140 kutoka wilaya za Tanganyika, Mpanda, Nsimbo, Serengeti, Uvinza, Kigoma, Simanjiro na Karatu.

(vii) Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu- Sekamaganga

36. **Mheshimiwa Spika,** Kituo kimetoa mafunzo kwa wanafunzi 204 ambapo Askari Wanyamapori wa Vijiji 20 wamepata mafunzo ya usimamizi wa rasilimasili za maliasili; na askari 150 wa TAWA wamepata mafunzo ya utayari wa Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu. Katika hatua nyingine, Kituo kimeandaa mitaala mipya ya kozi za Astashahada na Stashahada ya utalii na waongoza watalii.

(viii) Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania - TWPF

37. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko umeendelea kuwezesha operesheni maalum za kuzuia ujangili; utekelezaji wa kazi za Kikosi Kazi cha Taifa cha kupambana na ujangili (NTAP); na Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu. Aidha, Mfuko umewezesha kufanyika kwa uhakiki wa matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu katika wilaya 36 zilizoathirika pamoja na kufanya malipo ya Shilingi milioni 790.7 kwa wahanga 3,598 walioathiriwa na wanyamapori hao. Vilevile, Mfuko

umewezesha kuandaa mpango mkakati wa kuongoa Shoroba; na kuwezesha upatikanaji wa silaha za Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu.

**3.4.2 SEKTA YA MISITU NA NYUKI**

38. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Misitu na Nyuki ina jukumu la kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki. Katika mwaka wa fedha 2021, Wizara imetekeleza shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:-

39. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Mazao ya Mbao Yaliyohandisiwa (National Engineered Wood Sector Development Framework 2021 - 2031) pamoja na Mpango kazi wa utekelezaji wake utakaowezesha uanzishaji na uendelezaji wa viwanda vya mazao ya misitu hapa nchini. Pia, Wizara imefanya maboresho ya Kanuni ya tozo za mazao ya misitu ya mwaka 2020 na kuandaa Kanuni mpya toleo Na. 59 la mwaka 2022. Vilevile, Wizara imekamilisha ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao ya nyuki vitano (5) na ukarabati wa kiwanda kimoja (1) katika wilaya za Kibondo, Nzega, Sikonge, Bukombe, Mlele na Tabora Mjini.

(i) Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - TFS

40. **Mheshimiwa Spika,** Wakala umehakiki mipaka ya misitu 120 yenye urefu wa kilomita 160; kuweka vigingi 589 na mabango 204; kujenga barabara zenye urefu wa kilomita 49, kalavati nane (8) na daraja moja (1) katika mashamba ya miti 14 ya Buhindi, Kiwira, Longuza, Meru, North Kilimanjaro, Rondo, Rubare, Sao Hill, Shume, Mpepo, Ukaguru, West Kilimanjaro, Wino na North Ruvu. Aidha, wakala umeandaa mipango 48 ya usimamizi na uendelezaji wa misitu yenye ukubwa wa hekta zaidi ya milioni 1.2.

41. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wakala umezalisha tani 11.35 za mbegu bora za miti; kupanda miche zaidi ya milioni 9.8 katika eneo lenye ukubwa wa hekta 7,833; kupalilia hekta 19,601; kupogoa miti hekta 10,137; na kupunguza miti katika eneo la hekta 1,559. Kadhalika, kutoa mafunzo kwa watumishi 236 wanaofanya kazi ya kukabiliana na moto kwenye mashamba. Vilevile, katika jitihada za kusimamia na kuendeleza ufugaji nyuki, Wakala umezalisha tani 12.4 za asali na tani 0.3 za nta kutoka kwenye manzuki 182. Aidha, Wakala umeanzisha mashamba mawili (2) maalum ya kufuga nyuki ya Kondoa - Manyoni na Mwambao - Handeni. Vilevile, Wakala umetengeneza mizinga 2,500 na kuongeza mashine za kutengeneza mizinga katika kiwanda cha Wakala kilichopo Kondoa.

(ii) Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania - TAFORI

42. **Mheshimiwa Spika,** Taasisi imefanya utafiti kuhusu moto wa misituni na kubaini kuwa takriban eneo la kilomita za mraba 95,793 liliungua na moto kwa kipindi cha mwaka 2021/2022. Aidha, maeneo ambayo yameathirika zaidi na moto ni mikoa ya Lindi, Morogoro na Katavi. Pia, utafiti umebaini uwepo wa maeneo yaliyoathirika na matukio ya moto katika maeneo ya hifadhi kama vile Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba, Hifadhi za Misitu na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Vyanzo vikuu vya moto huo ni pamoja na ufunguaji mashamba kwa ajili ya kilimo, uvunaji asali usiotumia zana za kisasa, majangili na moto mpango.

(iii) Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki

43. **Mheshimiwa Spika,** Vyuo vya taaluma ya misitu na ufugaji nyuki vinajumuisha Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (BTI); Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI) na Chuo cha Misitu Olmotonyi (FTI). Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kimedahili wanafunzi 378 pamoja na kutoa elimu ya ufugaji nyuki wenye tija kwa wafugaji nyuki 130 katika wilaya za Sikonge, Mlele na Mpanda. Chuo cha Viwanda vya Misitu kimedahili wanafunzi 286, kuendesha programu ya mafunzo kazini kwa wahitimu 20 katika viwanda vitano (5) vya kuchakata magogo katika mikoa ya Iringa na Njombe; na kukarabati bwalo la chakula la wanafunzi. Kwa upande mwingine, Chuo cha Misitu Olmotonyi kimedahili wanafunzi 892 wa ngazi ya Astashahada na Stashahada.

(iv) Mfuko wa Misitu Tanzania - TaFF

44. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko umegharamia ununuzi wa mashine za kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki kwa ajili ya viwanda vinne (4) katika Halmashauri za Wilaya ya Kibondo, Bukombe, Sikonge na Mlele. Aidha, Mfuko umetoa ruzuku kwa miradi 60 inayoendelea na miradi mipya 63 ya uanzishaji wa vitalu vya miti na upandaji miti shuleni katika wilaya 36 za mikoa nane (8) inayopatikana katika maeneo ya Nyanda Kame ikiwemo Dodoma, Singida, Shinyanga, Simiyu na Manyara.

**3.4.3 SEKTA YA UTALII**

45. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Utalii ina jukumu la kusimamia, kuendeleza na kutangaza utalii nchini. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ilitekeleza majukumu yake katika sekta ya utalii kama ifuatavyo:-

46. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki iliandaa Onesho la Kwanza la Kimataifa la Utalii la Jumuiya ya Afrika Mashariki (East African Regional Tourism Expo - EARTE 2021) lililofanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 09 hadi 16 Oktoba, 2021. Katika hatua nyingine, Wizara ilishiriki Mkutano wa 64 wa Shirika la Utalii Duniani - Kamisheni ya Kanda ya Afrika (64th UNWTO Commission For Africa - CAF) uliofanyika kuanzia tarehe 02 hadi 04 Septemba 2021 katika Kisiwa cha Sal, Cabo Verde, ambapo Tanzania ilichaguliwa kwa mara ya kwanza kuwa Mwenyeji wa Mkutano ujao wa 65 wa UNWTO - CAF.

47. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya mapitio ya Sheria ya Utalii Sura 365 na kutangaza maboresho kupitia Tangazo la Serikali Na. 41 la mwaka 2021. Maboresho hayo yamewezesha kuondoa mamlaka ya Bodi ya Leseni katika kutoa leseni za wakala wa biashara za utalii nchini ambazo kwa sasa zinatolewa kupitia mfumo wa kielektroniki wa MNRT Portal. Sambamba na hilo, Wizara imetambua na kuhakiki huduma za malazi katika mikoa 26 Tanzania bara ambapo imeongeza idadi ya huduma zilizopaswa kukusanya tozo ya kitanda siku kutoka 1,815 mwaka 2020 hadi 8,681 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 378.

(i) Bodi ya Utalii Tanzania - TTB

48. **Mheshimiwa Spika**, Bodi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeratibu ushiriki wa Tanzania katika maonesho mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Maonesho hayo ni pamoja na FITUR 2022 na InvesTour ya nchini Uhispania; National Tour Association Annual Convention, nchini Marekani; road show iliyohusisha nchi za Ujerumani, Austria, Switzerland, Swedeni na Denmark; na Africa Tourism Leadership Forum 2021, nchini Rwanda. Aidha, Bodi iliratibu ushiriki wa Wizara katika onesho la dunia la Expo 2020 Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu, na uzinduzi wa Programu ya Royal Tour. Katika onesho hilo, nchi yetu ilipewa heshima ya pekee ya kuwa na siku maalum ambapo mnara maarufu duniani wa Burj Khalifa ulipambwa kwa rangi za bendera ya Tanzania; na vivutio vya utalii vilivyopo nchini vilioneshwa mubashara.

49. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya uteuzi wa mabalozi mbalimbali wa hiari akiwemo Bwana Mamadou Sakho, Raia wa Ufaransa ambaye ni mchezaji wa mpira wa miguu wa kimataifa wa Ufaransa; Bi. Rawan Dakik, aliyeweka rekodi ya kuwa mwanamke Mtanzania wa kwanza kupanda na kufika kwenye kilele cha Milima Everest, ambao ni mrefu zaidi duniani; Mtoto Sharon Ringo ambaye pia amepewa heshima ya kuwa Balozi wa Utalii katika Jumuiya ya Afrika Mashariki; na Bi. Isabella Mwampamba ambaye amekuwa akifanya shughuli mbalimbali za kuhamasisha na kutangaza utalii. Aidha, Wizara imeendelea kusambaza nyenzo za kutangaza utalii na kufanya vikao na wakala wa biashara za utalii pamoja na mabalozi wa nchi mbalimbali. Hatua hii imechochea watalii kutembelea nchini, mathalan, Tanzania imepokea makundi sita (6) yenye jumla ya watalii 1,924 kwa pamoja kutoka nchi ya Israel.

(ii) Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT

50. **Mheshimiwa Spika,** Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 1,127 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Aidha, Chuo kimekarabati miundombinu ya kutolea mafunzo katika kampasi za Bustani, Arusha na Temeke; na kununua na kusimika mifumo ya TEHAMA, vitendea kazi na vifaa mbalimbali vya kutolea mafunzo na kujifunzia katika kampasi za Mwanza, Temeke, Bustani na Arusha. Vilevile, Chuo kimenunua eneo lenye jumla ya ekari 32.2 kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya Mwanza.

**3.4.4 SEKTA YA MAMBO YA KALE**

51. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Mambo ya Kale ina jukumu la kusimamia uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za malikale na urithi wa utamaduni. Katika mwaka wa fedha 2021, Wizara imetekeleza shughuli mbalimali kama ifuatavyo:-

52. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kuenzi falsafa za Baba wa Taifa, Wizara imezindua Mpango wa Miaka 10 wa kuhifadhi kumbukumbu, kuenzi na kusherehekea Urithi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Katika kutekeleza mpango huo, Wizara imeratibu Adhimisho la Kumbukizi ya Miaka 100 tangu Kuzaliwa kwa Mwl. Nyerere kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali ikiwemo Taasisi za Elimu, Makundi ya Vijana, Asasi za kijami na wananchi kwa ujumla. Kilele cha Adhimisho hili kilifanyika tarehe 13 Aprili 2022 Mwitongo, Butiama- Mkoani Mara.

53. **Mheshimiwa Spika,** Ili kuimarisha Uhifadhi wa Malikale, Wizara imehakiki na kupima mipaka katika vituo saba (7) vya malikale vinavyosimamiwa na Wizara vilivyopo Mkoa wa Dar es Salaam, Tanga, Tabora, Iringa na Ruvuma. Wizara inaendelea na taratibu za kupata hati miliki katika maeneo hayo.

(i) Shirika la Makumbusho ya Taifa Tanzania – NMT

54. **Mheshimiwa Spika,** Shirika limekusanya mikusanyo 54 kutoka kutoka kwa jamii ya watu wa Songea na mikusanyo 25 kutoka kwa jamii ya watu wa Rukwa. Sambamba na hilo, ukusanyaji wa kumbukumbu za Marais wastaafu nchini umefanyika ikiwemo hotuba 79 zinazohusu ukombozi, maendeleo, uchumi utamadunia na siasa. Aidha Mikusanyo 1290 ya akiolojia imekusanywa kutokana na utafiti uliofanyika eneo la Laetoli lenye nyayo za Zamadamu. Ili kuendelea kutunza kumbukumbu hizi, Shirika limeandaa mfumo wa kidigitali wa kusajili na kuhifadhi mikusanyo na limejiunga na Datasaver ya National Internet Data center (NIDC). Katika hatua nyingine, Shirika limeweka onesho la kudumu la tembo katika Makumbusho ya Elimu Viumbe -Arusha; na usimikaji wa taswira za wanyamapori wakiwemo Nyati, tembo, twiga, faru na kiboko.

55. **Mheshimiwa Spika,** Shirika limefanya ukarabati wa jengo la kihistoria la Soko la Watumwa na kufungua ofisi katika Mji wa Mikindani. Aidha, Shirika limeanza kusimamia na kuendesha Kituo cha Makumbusho ya Dkt. Rashid Mfaume Kawawa kilichopo Songea. Vilevile Shirika limetoa elimu kwa jamii kuhusu urithi wa Utamaduni kwa kuendesha program 40 katika maeneo ya Madaba, Tunduru na Songea; kuanzisha klabu 35 za historia na uzalendo katika mikoa ya Tanga na Morogoro na kuendesha kampeni za Twenzetu Makumbusho, KijijiSoko na Museum Art Explosion.

(ii) Mfuko wa Mambo ya Kale

56. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko umewezesha maandalizi ya Mpango wa miaka 10 wa Kuenzi na Kusherehekea Urithi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere; ukarabati wa jengo alilofikia Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wakati wa kudai uhuru lililopo Manispaa ya Mikindani, Mtwara; kufanya tathmini ya Sera ya Malikale ya 2008; na kuwezesha uandaaji wa rasimu ya uwekezaji katika maeneo ya malikale.

**3.5 MIRADI YA MAENDELEO**

57. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022 Wizara imeendelea kutekeleza miradi mitano (5) ya maendeleo ambayo ni: Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Nyanda za Juu Kusini - REGROW; Mradi wa Kuzuia na Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara; Mradi wa Panda Miti Kibiashara; Mradi wa Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Misitu – FORVAC; na Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki – BEVAC. Kwa upande mwingine, Wizara ilitekeleza Mpango wa Maendeleo wa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya Athari za UVIKO-19 ambapo iliidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 90.2.

58. **Mheshimiwa Spika,** maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2021/2022 yamefafanuliwa kuanzia ukurasa wa 32 hadi ukurasa wa 104 katika Kitabu cha Hotuba.

**3.6 CHANGAMOTO NA UTATUZI**

**3.6.1 CHANGAMOTO**

59. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2021/2022, Wizara imekabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwepo wa ugonjwa wa UVIKO-19 duniani ambao umeathiri kwa kiasi kikubwa sekta ya utalii; ongezeko la migogoro kati ya binadamu na wanyamapori ambao umesababisha uharibifu wa mali, vifo na mlipuko wa magonjwa kati ya binadamu na wanyamapori. Changamoto nyingine ni; uwepo wa matukio ya moto katika maeneo ya hifadhi na uvamizi wa maeneo ya hifadhi kwa shughuli za kibinadamu; utegemezi

mkubwa wa misitu kwa ajili ya nishati; na uwepo wa mimea vamizi katika baadhi ya maeneo ya hifadhi.

**3.6.2 UTATUZI WA CHANGAMOTO**

60. **Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imeweka mikakati mbalimbali ikiwemo: kutoa elimu kwa wadau wa utalii juu ya namna bora ya kutumia Mwongozo wa Uendeshaji wa Shughuli za Sekta ya Utalii - SOPs; kujenga vituo vya askari katika maeneo yenye changamoto kubwa ya matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu; kutumia mbinu za kielektroniki za kufuatilia mienendo ya makundi ya wanyamapori wakali na waharibifu; kutoa elimu ya namna ya kujikinga na wanyamapori wakali na waharibifu; kuimarisha doria za kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara; kuendelea kutoa elimu ya namna ya kuzuia na kukabiliana na moto kichaa katika maeneo ya hifadhi; kuweka alama na mabango katika maeneo ya mipaka ya hifadhi; kuwezesha jamii inayopakana na maeneo ya hifadhi kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika maeneo yao; na kuwezesha miradi mbalimbali ya jamii ikiwemo ufugaji nyuki kwa lengo la kuwapatia kipato.

**4.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

61. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeandaa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2022/2023 kwa kuzingatia miongozo mbalimbali ikiwemo Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026); na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020 – 2025. Maeneo ya mpango huo ni Pamoja na:-

**4.1 Ukusanyaji Maduhuli**

62. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023, makadirio ya maduhuli yatakayokusanywa kutokana na sekta ya maliasili na utalii ni jumla ya Shilingi bilioni 670.86. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 469.36 zitakusanywa na Wizara kupitia mfumo wa TRA kutoka vyanzo vya TANAPA, NCAA na TAWA; na Shilingi bilioni 201.49 zitakusanywa moja kwa moja na Wizara kupitia mfumo wa MNRT Portal kutoka Idara, Mifuko na Taasisi nyingine za Wizara.

**4.2 Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

63. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa mwaka 2022/2023 inakadiria kutumia jumla ya Shilingi bilioni 624.14. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 443.70 zitagharamia Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni 180.44 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Makadirio ya Matumizi ya Kawaida yanajumuisha makadirio ya Mishahara Shilingi bilioni 175.88 na makadirio ya Matumizi Mengineyo Shilingi bilioni 267.82. Fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha Shilingi bilioni 109.88 fedha za ndani na Shilingi bilioni 70.56 fedha za nje.

**4.3 KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA NA WIZARA NA TAASISI ZAKE**

**4.3.1 SEKTA YA WANYAMAPORI**

64. **Mheshimiwa Spika,** Wizara itajenga barabara mpya zenye urefu wa kilomita 2,500 katika hifadhi za Taifa za Arusha, Burigi - Chato, Gombe, Katavi, Kilimanjaro, Kitulo, Mahale, Udzungwa, Manyara, Rubondo, Rumanyika - Karagwe, Ruaha, Mikumi, Nyerere na Serengeti. Aidha, Wizara itajenga njia za utalii zenye urefu wa kilomita 251 na barabara za kutembea kwa miguu zenye urefu wa kilomita 342.5. Vilevile, itakarabati barabara zenye urefu wa kilomita 6,500 na viwanja vya ndege 17 katika hifadhi za Taifa Ruaha, Mikumi, Nyerere, Saadani, Tarangire, Mkomazi na Serengeti. Aidha, itawezesha uandaaji wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi katika vijiji 30 vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa Nyerere na vijiji 18 vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa Serengeti; kuchimba mabwawa mapya nane (8); na kukarabati mabwawa matano (5) kwa matumizi ya wanyamapori katika hifadhi za Taifa za Mkomazi, Tarangire, Mikumi, Katavi, Ruaha, Saadani, na Serengeti. Pia, Wizara itaboresha maeneo ya malisho ya wanyamapori kwa kudhibiti mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 30,331 katika hifadhi za Taifa Nyerere, Saadani, Serengeti, Arusha, Ibanda-Kyerwa, Mto Ugalla, Mikumi, Mkomazi na Katavi. Vilevile, Wizara itaotesha miti ya asili 100,000 katika Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro.

65. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wizara itaendelea kuhamasisha ufugaji wa wanyamapori ili watu, makampuni na Mashirika binafsi waweze kuanzisha ranchi, bustani na mashamba ya wanyamapori. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza tafiti mbalimbali za kimkakati ikiwemo migongano baina ya binadamu na wanyamapori, mimea vamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa, chura wa Kihansi katika eneo lake la asili, utalii na maisha ya jamii Kusini mwa Tanzania. Aidha, Wizara itafanya sensa tatu (3) za wanyamapori katika maeneo ya Mfumo Ikolojia Nyerere - Selous - Liparamba - Mikumi, Mfumo Ikolojia Saadani - Wami Mbiki na Pori la Akiba Swagaswaga. Vilevile, Wizara itatoa mafunzo kwa wanafunzi 162 wakiwemo Askari Wanyamapori wa Vijiji (80), Waongoza Watalii (50) na Viongozi na wajumbe wa Kamati za Vijiji (32). Pia, itakarabati jengo la utawala, nyumba moja (1) ya watumishi na bweni moja (1) katika kituo cha mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu Sekamaganga.

**4.3.2 SEKTA YA MISITU NA NYUKI**

66. **Mheshimiwa Spika,** Wizara itaandaa mipango kazi ya kutekeleza Mikakati ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa za Misitu na Ufugaji Nyuki. Mathalani kuandaa mikakati ya Taifa ya Miti ya Mianzi; Kilimo Mseto; na Mkaa. Aidha, kuandaa miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Usimamizi wa Nyuki wasiouma. Pia, Wizara itaandaa Mipango ya Usimamizi wa Misitu 57 yenye ukubwa wa hekta 1,703,202 na kufanya mapitio ya Mipango ya Usimamizi wa misitu ya hifadhi 111. Vilevile, kuweka vigingi 1,369 na mabango 2,133; na kujenga minara miwili (2) mipya ya kubaini matukio ya moto na kukarabati mingine 11. Kwa upande mwingine, Wizara itaanzisha shamba jipya moja (1) la ufugaji nyuki; kuzalisha tani 49 za asali, tani 2.9 za nta na kilo 50 za chavua; na kuchonga mizinga ya nyuki 1,200.

67. **Mheshimiwa Spika,** Wizara itafanya tafiti za kimkakati sita (6) zenye lengo la kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya misitu na nyuki nchini. Aidha, Wizara itaanzisha Utalii wa Nyuki kupitia Manzuki za Chuo cha Ufugaji Nyuki Tabora; kujenga bweni katika Chuo cha Viwanda vya Misitu, na kukarabati mabweni sita (6) na nyumba za wakufunzi 10 katika Chuo cha Misitu Olmotonyi. Sambamba na hilo, Wizara itawezesha utekelezaji wa miradi 209 inayoendelea na miradi mipya 180 ya uanzishwaji wa vitalu vya miti; upandaji miti mashuleni; na ufugaji nyuki.

**4.3.3 SEKTA YA UTALII**

68. **Mheshimiwa Spika,** Wizara itakamilisha Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Utalii ya Mwaka 1999; na kuandaa Programu ya Maendeleo ya Utalii nchini. Aidha, itabainisha maeneo ya fukwe katika maziwa makuu ya Viktoria, Tanganyika na Nyasa kwa ajili ya uwekezaji na uendelezaji wa shughuli za utalii. Katika hatua nyingine, Wizara itaendelea kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora katika mikoa ya Kilimanjaro, Mbeya na Mwanza. Sambamba na hilo, Wizara itabaini vivutio vya utalii na fursa za uwekezaji wa shughuli za utalii nchini katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, Morogoro na Tanga.

69. **Mheshimiwa Spika,** Wizara itaandaa mkakati wa uendelezaji wa utalii wa mikutano na matukio; onesho la sita (6) la Swahili International Tourism Expo (S!TE); na kuratibu Mkutano wa 65 wa Shirika la Utalii Duniani - Kamisheni ya Kanda ya Afrika (UNWTO 65th CAF Meeting). Aidha, itaratibu ziara maalum 15 za mafunzo kwa ajili ya makundi maalum ya wadau ikiwemo wakala wa biashara za utalii, waandishi wa habari, watu mashuhuri, mabalozi wa hiari wa utalii na wawekezaji katika masoko mbalimbali ya utalii. Sambamba na hilo, kuratibu na kushiriki katika matukio yanayohusisha utangazaji utalii ndani ya nchi pamoja na kuendeleza juhudi zilizoanzishwa kupitia programu ya Tanzania – The Royal Tour. Kwa upande mwingine, Wizara itakarabati miundombinu ya kutolea mafunzo katika Chuo cha Taifa cha Utalii Kampasi ya Bustani, Temeke na Arusha.

**4.3.4 SEKTA YA MAMBO YA KALE**

70. **Mheshimiwa Spika,** Wizara itafanya tathmini ya utekelezji wa Sera ya Malikale ya mwaka 2008 na kuandaa mkakati wa utekelezaji; na kufanya mapitio ya Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333 na Sheria ya Makumbusho ya Taifa Sura 281. Aidha, Wizara itaandaa kanuni na miongozo ya uhifadhi na utafiti wa maeneo ya malikale; vigezo vya kutambua rasilimali za Urithi wa Utamaduni kuwa Urithi wa Taifa; na mpango wa kitaifa wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za urithi wa utamaduni. Katika hatua nyingine, Wizara itapima maeneo saba (7) ya malikale; na kutengeneza mfumo wa maombi ya vibali vya utafiti. Sambamba na hilo, Wizara itafanya ukarabati wa majenzi ya kale 22; kufanya tafiti nne (4) na kukusanya na kuhifadhi mikusanyo ya asili na kiutamaduni 220. Vilevile, Wizara itakusanya taarifa za maeneo mapya ya malikale katika mikoa ya Katavi, Simiyu, Njombe, Dodoma, Kigoma na Lindi. Pia, itawezesha uandaaji wa mpango wa uhifadhi wa mji wa kihistoria wa Bagamoyo na Pangani.

**4.4 MIRADI YA MAENDELEO**

71. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara itatekeleza miradi ya maendeleo ambayo ni: Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini; Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma; Mradi wa Kukabiliana na Ujangili na Biashara Haramu ya Wanyamapori; Mradi wa Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi Ujangili; Mradi wa Panda Miti Kibiashara; Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki; Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki; Mradi wa Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio; na Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa dhidi ya UVIKO-19.

72. **Mheshimiwa Spika,** maelezo ya kina kuhusu shughuli na miradi itakayotekelezwa katika Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023 yamefafanuliwa kuanzia ukurasa 106 hadi ukurasa 141 katika Kitabu cha Hotuba.

**5.0 SHUKRANI**

73. **Mheshimiwa Spika**, ninapenda kutumia nafasi hii tena kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa ushirikiano mnaotoa katika kuliongoza Bunge letu Tukufu. Pia, ninawashukuru wadau wote kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kipekee, nizishukuru nchi marafiki, washirika wa maendeleo, mashirika ya kimataifa, taasisi za kiserikali pamoja na wadau wengine wakiwemo sekta binafsi kwa ushirikiano wao katika kuendeleza Sekta ya Maliasili na Utalii na uchumi wa nchi kwa ujumla. Nachukua fursa hii kutaja baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Canada, China, Falme za Kiarabu, Korea Kusini, Marekani, Morocco, Namibia, Norway, Ubelgiji, Ufaransa, Ufini, Ujerumani, Uswisi na Jumuiya ya Umoja wa Nchi za Ulaya. Mashirika na taasisi za Kimataifa ni pamoja na: AfDB, AWF, AWHF, FAO, FZS, GEF, GIZ, ICCROM, ICOM, ICOMOS, ILO, IMF, ITC, IUCN, KfW, NORAD, PAMS Foundation, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UNWTO, USAID, WCS, WHC, WTTC, World Bank, Wild Aid, WMF na WWF. Aidha, ninapenda kuwashukuru wananchi wote walioshiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi wa maliasili, malikale na uendelezaji utalii. Nitumie fursa hii kuwaomba wadau wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

**6.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023**

74. **Mheshimiwa Spika,** ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 624,142,732,000 (bilioni mia sita ishirini na nne, milioni mia moja arobaini na mbili, mia saba thelathini na mbili elfu) kwa matumizi ya Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kati ya fedha hizo, Shilingi 443,706,567,000 (bilioni mia nne arobaini na tatu, milioni mia saba na sita, mia tano sitini na saba elfu) ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 180,436,165,000 (bilioni mia moja na themanini, milioni mia nne thelathini na sita, mia moja sitini na tano elfu) ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

75. **Mheshimiwa Spika,** fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha Shilingi 175,884,707,000 (bilioni mia moja sabini na tano, milioni mia nane themanini na nne, mia saba na saba elfu) za mishahara na Shilingi 267,821,860,000 (bilioni mia mbili sitini na saba, milioni mia nane ishirini na moja, mia nane sitini elfu) za matumizi mengineyo. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha Shilingi 109,879,593,000 (bilioni mia moja na tisa, milioni mia nane sabini na tisa, mia tano tisini na tatu elfu) fedha za ndani na Shilingi 70,556,572,000 (bilioni sabini, milioni mia tano hamsini na sita, mia tano sabini na mbili elfu) fedha za nje.

**7.0 HITIMISHO**

76. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Aidha, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii: www.maliasili.go.tz.

77. **Mheshimiwa Spika,** naomba hotuba yangu yote iingie kwenye hansard za Bunge kwa ajili ya kumbukumbu.

78. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Safari yetu; Kutoka zama zile za kula sinia moja, hadi kujipakulia

## •Wenye enzi walia 'ya leo ubinafsi mtupu'



Na Adam Fungamwango

KILA kukicha kwenye vyombo vya habari tumekuwa tukisikia matukio kadhaa makubwa, yakiwamo mauaji.

Makanda wa Polisi sasa mikoa mbalimbali wamekuwa na kazi ya kusimama kwenye vyombo vya habari kutangaza kwa huzuni, matukio kadhaa mabaya kwenye jamii ambayo miaka ya nyuma, yalikuwa machache mno na ya kuhesabu.

Na hata yalitokea, inakuwa simulizi ambayo haisahauliki kirahisi. Ukiingia kwenye mitandao ya kijamii, kufungulia televisheni, redio au kusoma magazeti, inabidi uwe na moyo mgumu, kwani badala ya kukutana na habari nyingi za kuelimisha na kuburudisha, unakutana pia na habari za kutisha na kusikitisha.

Ndiyo tunaona mume kamuua mkewe, mtoto kamuua baba au mama, mzazi katupa kichanga, dada wa kazi kamuua mtoto wa bosi wake, mwanamke kachoma moto nyumba ya mpenzi wake, baba kambaka binti yake, wengine wanaua wazazi wao kwa sababu wanachelewa kufa ili wao wapate urithi na nyingine nyingi ambazo badala ya kukufanya ufurahie habari, zinazidi kukutia simanzi.

Ni wakati ambao hata wafanyakazi na baadhi ya viongozi wamekosa uzalendo kwenye taasisi zao au nchi.

Rushwa, wizi, upendeleo umekithiri. Mtu badala ya kufanya kazi kwa manufaa ya taifa, anafanya kwa manufaa yake binafsi na familia yake.

Utakuta kuna watu wanailaumu serikali kwa yote yanayotokea. Wengine wanasema eti hali ya maisha ni ngumu, ndiyo maana haya yote yanatokea.



Nadhani ni kizazi cha miaka ya karibuni ndiyo wanasema haya, kwa sababu sijui kama hali mbaya ndiyo inasababisha watu wafanya mambo haya, sijui ingekuwaje enzi za uhaba wa unga, sukari, mchele, sabuni, dawa ya miswaki na dawa ya mbu pia miaka ya mwanzoni mwa 1980.

Tatizo hapa wala si serikali, ni kwamba wazazi wengi ndiyo chanzo cha yote haya, kutokana na aina ya malezi ya kisasa kwa watoto wetu.

Ndiyo wanayofanya wawe makatili, wasio na huruma, ubinafsi na kukosa uzalendo.

Mfano mdogo ni nitawapa. Asubuhi moja nipo kwenye daladala, kwa bahati nzuri nimefanikia kupata siti na kukaa.

Baada ya kuketi kwenye kiti na gari kuanza safari, nikamuona mama mtu mzima mwenye umri usiopungua miaka sabini mpaka themanini kasoro akiwa amesimama kwa kujikunja kutokana na uchovu wa utu uzima wake huku chini yake akiwa ameketi binti wa miaka isiyozidi 22 hivi.

Hakuhangaika wala kumtazama bibi yule, badala yake alikuwa anahangaika na simu yake janja.

Labda kwa sababu mimi ni mmoja wa watoto niliolelewa enzi zile, moyo wangu ukashtuka kwa fedheha na huruma nikijikuta namwita yule mama mtu mzima kwa sauti ya upole

"Mama njoo ukae hapa"

Mama akanionyesha uso wa tabasamu kisha akasogea nikampisha akakaa na mimi nikasimama.

Kwa bahati mbaya hakuna hata abiria mmoja aliyediriki kumkosoa au kumwelimisha yule binti kwa kile kitendo alichokifanya kila mmoja alikuwa bize na simu yake na wengine wakiendelea kupiga soga. Tukio hilo lilionekana la kawaida tu.

Ndiyo kizazi chetu cha sasa kilivyo. Malezi ya kudekezana na kuwaachia madada wa kazi kulea watoto ndiyo waliokifikisha kizazi hiki hapa.

Wazazi wengi wa sasa utawasilia wakisema "sitaki kumwona mtoto wangu akitaka shida kama nilizopata mimi."

Wao wanadhani malezi waliyoyapata kwa wazazi wao walikuwa ni ya 'mkono wa chuma', na wala si ya kuwatengeneza na kuwa watu bora kwenye jamii.

Si ajabu leo na wala si mara moja wala mbili nimepanda kwenye daladala na kumkuta baba au mama amemlipia mtoto au watoto wake siti wamekaa, lakini hapo hapo kuna babu au bibi amesimama.

Hapo mtoto anafundishwa nini kama siyo ubinafsi? Huyu anaweza kumheshimu mtu mwingine yoyote au kumjali atakapokuwa mkubwa?

Zamani kitu kama hiki kilikuwa hakuna. Hakuna mtoto yoyote anayeweza kukaa kwenye kiti au siti ya gari wakati mkubwa amesimama.

Zamani watoto wote wa familia moja walikuwa tunakula kwenye sahani moja. Wakati mwingine wao wenyewe au na wazazi wao.

Hii ilisaidia kuimarisha upendo na umoja miongoni mwa watoto wenyewe, lakini baba au mama waliweza kugundua makosa mbalimbali ya watoto wao na kuyarekebisha.

Atagundua kwenye kisirani, mchoyo, mgomvi, anayekula matonge makubwa ili awazidi wenzake, anayependa kula nyama zaidi kuliko chakula chenyewe, mkomba mboga, wa kwanza kula nyama, anayependa kuongeaongea wakati wa kula, na kasoro nyingi za watoto kabla ya kuzirekebisha.

Pia waliweza kujua hata afya za watoto wao, kwani anaweza kumuona kwenye kidonda, punye, kipele, magonjwa mengine ya ngozi, kukohoakohoa, chanya mara kwa mara, kushindwa kuhema vizuri na hata kugundua anayeshindwa kula vizuri.

Hapa wazazi wanakuwa wameshapata pa kuanzia kurekebisha au kutibu chochote kile ambacho watakiona ni kasoro kwa mtoto au watoto wake.

Leo hii wazazi wengi hawana tena mfumo huu wa malezi bali kila mtoto ndani ya familia anakula katika sahani yake peke yake. Kila mtu anapakua chakula kilichoko kwenye chombo maalum cha kuhifadhia chakula kisha kila mmoja anakimbilia upande wake. Mwingine ataenda kulia barazani, mwengine uwani, mwengine chumbani na mwengine sebuleni, ili mradi tu shaghalabaghala.

Tayari utaona mfumo huu unalazimisha kuwatenganisha watoto. Hawawezi kuwa na umoja na upendo kama wale wa zamani.

Kila mmoja anakuwa anajijali mwenyewe. Ubinafsi unaanza kuzaliwa. Hawa hata kama wakikua na mmoja kuanza kujitegemea watakuwa wanasaidiana kwa shida na raha.

Watakuwa wanawasiliana kwenye simu tu. Itafikia wakati huko mbele itakuwa kama nchi zilizoendelea, watakuwa hawawalei hata wazazi wao. Watakuwa wakiwapeleka kwenye vituo vya kulelea wazee.

Kwa sababu hizo ndizo tabia za watu wabinafsi. Ni kwamba wazazi wenyewe wanajitegea mabomu ambayo yatakuja kuwalipukia baadaye.

Hata uzalendo kwenye nchi umeshuka, hauko kama zamani. Ni kwa sababu ya ubinafsi tu ambao unazaa roho mbaya, chuki, ukatili na hata rushwa.

Mtu analijilimbikizia mali, akiiba mali ya shirika au taasisi kwa sababu hata uchungu na nchi, wala wananchi, bali yeye na familia yake tu.

Maisha ya uzungu ndiyo wametuponza. Haya tulikuwa tunayasikia barani Ulaya na Amerika. Kwa sababu ya aina yao ya maisha ya ubinafsi na upweke. Ndiyo utaona mtu anawapiga risasi wenzake shuleni.

Kwa sasa taratibu yanaanza kushuka Afrika. Kwa sababu ya kuiga maisha yao. Nadhani wazazi hawajachelewa, wanaweza kujirekebisha.

**Tuma meseji: 0716 350534**

## HABARI KIMATAIFA

# Biden awataka wabunge kuchukua hatua

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani, Joe Biden, amesema juhudi zilizoko za kudhibiti matumizi ya bunduki, hazilengi kumnyang'anya mtu silaha.

Biden alisistiza kwamba maeneo mengi nchini humo kila siku yanageuka kuwa viwanja vya mauaji.

Akizungumza katika Ikulu ya Marekani, kiongozi huyo alisema hakuna chochote kilichofanywa baada ya mauaji ya watu wengi ya kutumia bunduki, lakini lazima wachukue hatua.

Biden alisema ameshangazwa na hatua ya wabunge wengi wa Chama cha Republican katika Baraza la Seneti kukataa kuchukua hatua yoyote kuhusu sheria ya mashambulizi ya kutumia bunduki na umiliki wake.

# UN: Wakimbizi Myanmar zaidi ya milioni moja

**NEWYORK,** MAREKANI

SHIRIKA la Huduma za kiutu la Umoja wa Mataifa, limesema kwa mara ya kwanza idadi ya raia wa Myanmar waliokimbia makazi yao imepindukia milioni moja.

Taarifa hiyo ilisema nusu ya idadi hiyo wamepoteza makazi baada ya jeshi kuchukua udhibiti mapema mwaka jana.

Ofisi hiyo ya uratibu ya Umoja wa Mataifa, (OCHA) ilisema kwenye ripoti yake kwamba hali tete ambayo tayari ilikuwapo inayochochewa na mapigano yanayoendelea kati ya vikosi vya serikali na wapinzani wake.

Ripoti hiyo ilisema zaidi ya watu 694,300 wamelazimishwa kuwa wakimbizi wa ndani huku karibu watu 346,000 walikimbia kutokana na mapigano kabla ya jeshi kuchukua udhibiti.

# Siku 100 vita Ukraine na Russia

## ● Russia yafanikiwa kuteka ardhi 20%
## ● Ulaya yagawanyika vikwazo vya mafuta

VITA kati ya Russia na Ukraine imefikisha siku 100 jana tangu kuanza Februari 4, huku ikiripotiwa mapigano makali yanaendelea mashariki mwa nchi hiyo.

Hata hivyo, tayari Ukraine imethibitisha kupoteza asilimia 20 ya ardhi yake baada ya vikosi vya Russia kuchukua baadhi ya maeneo ya Crimea, Pariupol na sasa Donbas.

Baada ya kushindwa katika azma yao ya kuuteka mji mkuu Kyiev, majeshi ya Urusi yameelekeza nguvu katika kuiteka Ukraine mashariki jambo ambalo huenda likasababisha mzozo huo kuwa wa muda mrefu.

**RUSSIA YAANZA MAZOEZI KIJESHI PACIFIC**

Jeshi la Russia la Pacific Fleet limezindua mfululizo wa mazoezi ya wiki moja huku meli zaidi ya 40 na ndege 20 zikishiriki.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Ulinzi, ilisema mazoezi hayo yanafanyika katika mkakati wa kuimarisha ulinzi wa majini.

Ilisema mazoezi hayo, yanayofanyika kuanzia Juni 3 hadi 10 na kuhusisha meli ambazo zinafanya kazi ya kutafuta meli za adui.

**UKRAINE YAPATA MAFANIKIO KATIKA MAPAMBANO**

Mapigano makali yanaendelea katika mji wa Severodonetsk eneo la Donbas ambapo asilimia 80 ya eneo hilo tayari limeshatekwa na Russia.

Hata hivyo, majeshi ya Ukraine yanaweka upinzani mkali na kumfanya Rais Volodymyr Zelenskiy, kusema kwamba nchi yake imepata ufanisi kiasi katika mapambano hayo ya mashariki.

**MWENYEKITI WA UMOJA WA AFRIKA, AKUTANA NA PUTIN**

Rais wa Senegal ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika (AU), Macky Sall amekutana na kiongozi wa Russia, Vladimir Putin na kufanya mazungumzo.

Katika ziara hiyo Sall, ameandamana na Rais wa Kamisheni ya umoja huo, Moussa Faki Mahamat.

Mkutano huo ni mpango wa kwanza wa kidiplomasia wenye lengo kuu la kukomboa akiba ya nafaka na mbolea, ambayo imeathiri nchi za Kiafrika pamoja na kupunguza mzozo wa Ukraine.

Russia na Ukraine pekee zinauza nje asimilia 30 ya ngano inayouzwa duniani.

Bei ya nafaka barani Afrika, imepanda kwa sababu ya kudorora kwa mauzo ya nje kutoka Ukraine, na hivyo kuongeza athari za migogoro na mabadiliko ya hali ya hewa na kuzua hofu ya machafuko ya kijamii.

Kampeni ya kijeshi nchini Ukraine na msururu wa vikwazo vya kimataifa dhidi ya Russia vimetatiza usambazaji wa mbolea, ngano na bidhaa nyingine kutoka nchi zote mbili, na kupandisha bei ya chakula na mafuta.

Senegal ni mojawapo ya nchi 35 ambazo hazikupiga kura katika azimio la Umoja wa Mataifa, kudai kwamba Russia iache mara moja kutumia nguvu dhidi ya Ukraine.

**ULAYA YAGAWANYIKA VIKWAZO VYA MAFUTA**

Umoja wa Ulaya (EU) katika mkutano wake wa jana umeidhinisha rasmi vikwazo vya mafuta dhidi ya Russia na vikwazo vingine vinavyolenga benki kubwa na watangazaji kufuatia uvamizi wake nchini Ukraine.

Taarifa kutoka makao makuu ya umoja huo, ilisema mafuta ghafi ya Russia yataondolewa katika kipindi cha miezi sita na miezi minane kwa bidhaa nyingine za mafuta yaliyosafishwa. Ilisema hatua hiyo kwa sasa haitayahusu mataifa yasiyo na bahari kama Hungary, Jamhuri ya Czech na Slovakia ambayo yalipinga vikwazo hivyo kutokana na kutegemea usambazaji kutoka nchi hiyo.

Bulgaria na Croatia pia zitatengwa kwa muda kwa baadhi ya bidhaa za mafuta.

Wakuu wa Ulaya walisema hatua hiyo inamaanisha kwamba karibu asilimia 90 ya usambazaji wa mafuta kutoka Russia kwenda katika bara hilo itakuwa imezuiwa ifikapo mwishoni mwa mwaka.



Malkia wa Uingereza akikata keki kusherehekea miaka 70 ya utawala wake katika makazi yake Buckingham, London juzi. **PICHA: DW**

# Marekani yalalamikia Russia, China kujitenga

**SEOUL,** KOREA KUSINI


MAREKANI imesema China na Russia hazina mpango wa kushirikiana nao katika kudhibiti Korea Kaskazini na mipango yake ya nyuklia.

Taarifa kutoka ujumbe wa nchi hiyo kuhusu nyuklia, ulisema hayo baada ya nchi hizo mbili kupiga kura ya turufu dhidi ya pendekezo la Marekani la vikwazo vipya kwa Korea Kaskazini. Kwenye mikutano inayofanyika Seoul kati yao na Korea Kusini na Japan, mwakilishi maalumu wa Marekani, Sung Kim alisema ni hiari ya China na Urusi kushirikiana na Marekani, ambayo bado inatazamia kuwapo mazungumzo na mataifa hayo mawili ili kuongeza mbinu kwa Korea kaskazini.

Maofisa hao wamekutana kujadiliana kuhusu nchi hiyo kutokana na mashaka kwamba taifa hilo lililotengwa linajiandaa kufanya jaribio jingine la nyuklia kwa mara ya kwanza tangu mwaka jana.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MAXIMILLIAN E. MAHIZI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye **INDEX NAMBA S4692-0656** kilichotolea na Baraza La Mitihani La Taifa kupitia **ST. JOSEPH'S CATHEDRAL SECONDARY SCHOOL** mwaka **2018**. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:**
**DSM/PHQ/RB/192079/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GODFREY GODFREY KAHWILI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye namba za usajili **T999DEK. Chassis No. SR400266611**, Engine No. **3S8025715**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya polisi:**
**DOD/DOD/RB/209666/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ADAMSON PETER MJEMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye namba za usajili **T924DUV. Chassis No. NCP110-0018526**, Engine **No. 1NZD296911.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya polisi:**
**DOD/DOD/RB/219237/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JASMIN HASSAN MUSHY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye USAJILI **NAMBA T580 AUV** na **CHASSIS NAMBA: ST2100042387.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:**
**ARU/ARU/RB/26228/2022**

*Magistrate Court (approved forms for the Primary Court)*
*GN.NO.943 (Contd.)* *FOMU MADAI-3*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya Wilaya Kigoma**
**Kituo cha Ujiji**
**Mkoa wa Kigoma**
**SHAURI LA MADAI NA 113/20......MWAKA.......2022**
**JINA LA MDAI. KAMANGA KASANGA WATENDELE**
**JINA LA MDAIWA. NAIMANA STUMAI NA MWENZAKE MMOJA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
*(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo).*

Kwa.................. NAIMANA STUMAI ............
Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba (eleza habari za madai).............anakudai kiasi cha fedha Tsh. 8,000,000/= kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe...08....Mwezi...06....Mwaka...2022....... saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikathibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe.....01.....Mwezi....06...Mwaka.....2022...........

..............................
**HAKIMU**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ZAKARIA WILFRED** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **INDEX NAMBA: S0329-0173** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MAKUMIRA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2009.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: DAR/MBA/RB/486716/2019**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SILVESTER DAMAS SAGAMBA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye **USAJILI NAMBA T827 CMN , CHASSIS NAMBA : ACA210046658 na ENGINE NAMBA: 1AZ0159389.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**POLISI TAARIFA :**
**DAR/URA/B/148428/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**CHRISTINA PHILEMON MWANYONGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE **INDEX NAMBA PS 3791/0017** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI KUPITIA LYOTO SEKONDARI MWAKA 2013.YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.**TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/4878/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya GEITA**
**Kituo cha NYANKUMBU**
**mkoa GEITA**
**Shauri la madai/ ndoa Na. 80/2022**
**Jina la mdai GEORGE ALEXANDER MPOGOLOMI**
**Jina la mdaiwa RYUBA PAULO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
*(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo)*

**Kwa**
**RYUBA PAULO WA GEITA**
Kwa kuwa mdai/ wadai amelata/wameleta madai yake/yao kwamba ( eleza hapa habari za madai)
Unatakiwa kuhudhuria mahakamani hapa bila kukosa au kuchelewa ili kujibu madai dhidi yako ya 8,500,000/=. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 9 mwezi 6 mwaka 2022 saa 2:00 asubuhi/ mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
ANGALIZO: kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 02 mwezi 06 mwaka 2022

RESIDENT MAGISTRATE GEITA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AMANI .A. NGUME**
Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya **GARI(ISUZU)** yenye Chassis no. **7109313** na namba za usajili **T 957 AJH** yeyote atakae iyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba
**0712789741**
**MOR /MOR/B/159298/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya**
**Mwanzo ya Wilaya ya ............TANGA**
**Kituo cha..... MJINI TANGA.... Mkoa... TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi............113/2022............**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: PAYO MOHAMED ZAMU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA: FATUA YUSUFU HUSSENI**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslai yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 24/6/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetolewa leo 3/6/2022**

HAKIMU

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**IMANI LAMECK KIRENGA**
Anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne index No S.2421/0089Mwaka 2017 Shule ya Sekondari STAR HIGH SECONDARY SCHOOL, kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**Taarifa polisi: DOD/DOD/RB/113716/2022.**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**JEREMIAH ASAM AMOLO**
Mtajwa hapo anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria (passport) Yenye namba AB936850. Kwa atakae iona atoe taarifa Kituo chochote cha polisi kilichopo karibu kwa Kumb:
**MWA/NYA/RB/217072/2022.**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu **FIRST NATIONAL BANK** tutauza kwa mnada wa hadhara mali/dhamana ya mdaiwa wa Benki, kama ilivyoorodheshwa hapo chini, mnada utafanyika kama ifuatavyo: -

- **NYUMBA ILIYOPO KIWANJA NA. 244, KITALU '12', C.T NA 61388, ENEO LA MBWENI MPIJI, MALI YA ABDULKADIR ABDU MGHENI, MNADA UTAFANYIKA TAREHE 18 JUNE 2022 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI NA KUENDELEA**

**MASHARTI YA MNADA**
Mnunuzi anatakiwa kulipa asilimia 25% ya bei itakayofikiwa siku ya mnada na salio la asilimia 75% anatakiwa kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia siku ya mnada.
Mnunuzi akishindwa kulipa salio la asilimia 75% ndani ya siku kumi na nne (14) atakuwa amepoteza haki zake zote pamoja na asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
Nyumba inaweza kukaguliwa kuanzia tarehe ya tangazo hili mpaka siku ya mnada.
Mnunuzi anatakiwa kusimamia mwenyewe zoezi la kubadili hati ya kumiliki/mali aliyonunua na kulipa kodi zote stahiki.
Nyumba/mali itauzwa mahali na kama ilivyo

Wote mnakaribishwa
**Kwa mawasiliano:**
**FIRST NATIONAL BANK MM AUCTIONEERS& DEBT COLLECTORS CO.LTD**
**FNB HOUSE, OHIO STREET, S.L. P 20306, DAR ES SALAAM**
**P.O.BOX 72290, DAR ES SALAAM , SIMU: 0755 404 801/ 0715 401 801**

*Uza,*
*Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*
*Tupigie*
*0782253676*

# KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-8

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Baada ya kuambiwa kuwa mgeni Bakari si mpenzi wake, basi alijua anaweza kukubali ombi la huyo aliyemtuma.

"Mmh, sasa nikamwambieje?"

"Bibi wee, nenda kamwambie hivyo hivyo kama alivyokutuma. Simtaki."

"Siwatu, ukikataa sasa si watu watasema yule mgeni ndiyo mpenzi wako? Maana Maiko kasema yuko tayari hata kukuoa."

"Hahahaa" Siwatu alicheka kicheko cha hasira kilichochanganyikana na dharau. "Anioe mimi Maiko? Wapiii, yaani kabisa na akili zake, kakaa huko kafikiria, kakuita kakwambia nenda kakwambie Siwatu nampenda, tuwe wapenzi na ikiwezekana nitamuoa he he..."

"Basi, mimi nitamrudishia hilo jibu lake." Mage alijibu kwa upole na aibu.

"Tena kamwambie, anione kama chongo la mkwewe, akiniona asinisemeshe, wala kupita karibu na mimi. Kwanza nashangaa watu wamenitenga, wamenisusa, sasa yeye kilichomfanya ajishaue nini?"

"Sawa, sasa nimwambie ana mtu au?"

"Eee bibi wewe nawe usinit'bue, niwe ninae niwe sina, haikuhusu, mlango ulioingilia ndiyo huo huo tokea. Kwambie chochote kile, lakini simtaki. Na hili suala na kudhani kama itaonekana Bakari ndiyo mpenzi wangu mimi halinisumbui. Mbona wote kijijini wanajua kuwa ni mpenzi wangu wakati siyo." Siwatu alionekana kama vile amefikia kilele cha hasira.

"Eee, basi yameisha." Akajibu Mage huku akiinuka tayari kwa kuondoka.

"Asikutume tena, na wewe usikubali tena kutumwa na huyo mtu wako, tena kamwambie, iwe mwanzo na mwisho."

Siwatu alisimama mlangoni na kumwangalia kwa hasira na dharau Mage aliyekuwa anaondoka taratibu.

"Msichana usiyetaka kukaa kwako unamsaidia mama yako kufua au kupika, kazi kiguu na njia tu kwa umbea, lo..." Akaongea kwa sauti ya chini ambayo isingeweza kusikika na mtu yoyote zaidi ya yeye mwenyewe.

**************************

"Mwenzetu mbona hivyo unaumwa?"

"Hapana."

"Mmmh, siyo kweli, unaumwa, au kama siyo kuna kitu kinakutatiza."




**"Nimeota hali si shwari huko nyumbani. Nimeota kama kuna vilio, na nimekuwa nikitajwa mimi kwenye ndoto hiyo. Na nilipoamka usiku, nikakaka tena, nikaona kitu kinachofanana tena na hicho."**

"Hapana Siwatu."

"Siyo kweli Bakari, mimi kwa muda wa miezi mitatu naishi na wewe hapa, sikufahamu ulivyo kweli?"

"Kwani leo nikoje?"

"Hapana bwana wewe hauko hivyo, ni mtu mchangamfu na mwepesi kufanya jambo lolote, lakini leo naona mzito, unajivuta, halafu huongei, kama unashangashangaa hivi, imekuwaje?"

Bakari alijitahidi kutabasamu, lakini mdomo uligoma.

"Unaona sasa, unataka hata kutabasamu, lakini unashindwa. Kama unaumwa, nikakuchumie dawa, au kama ni ugonjwa mkubwa kidogo, twende kwenye zahanati ya kijiji jirani." Akasema Siwatu huku macho yakiwa yamemtoka.

Siku zote ameishi na Bakari, amekuwa akifarijika na kuwepo kwake, kutokana na jinsi walivyokuwa wakiishi.

Kwa nje walionekana ni kama mtu na mpenzi wake. Lakini wakiwa ndani ni kama mtu na dada yake. Hakugusana. Ingawa utani wa hapa na pale ulikuwa ukiendelea, kila mmoja akimheshimu mwenzake.

Kwa sababu walikuwa wakilala kwenye nyumba moja, watu wote walijua kuwa ni mtu na mpenzi wake.

Siri ya kwamba si wapenzi, walikuwa wanaijua wenyewe tu.

"Ni kweli dada kuna kitu." Akajibu na kumfanya Siwatu kuhisi kama kuna kitu kimempiga kwenye moyo wake.

"Nini niambie." Akasema huku akihema.

"Siumwi kama unavyofikiria, ila nimeota ndoto mbaya." Jibu hilo lilifanya moyo wa Siwatu utulie, lakini bado alikuwa na shauku ya kutaka kujua ndoto hiyo inahusu nini. Kabla hata hajauliza Bakari aliendelea.

"Nimeota hali si shwari huko nyumbani. Nimeota kama kuna vilio, na nimekuwa nikitajwa mimi kwenye ndoto hiyo. Na nilipoamka usiku, nikakaka tena, nikaona kitu kinachofanana tena na hicho."

"Mhh, mwenzangu pole sana, sasa..." "Nimeamua kitu kimoja ambacho kitakuwa kigumu sana kwangu. Kuondoka." Neno kuondoka lilimlipua tena moyo Siwatu.

"Unaondoka?" Akauliza kana kwamba hajasikia.

"Nimeamua niende kwanza nyumbani nikaangalie kama wazazi wangu watakuwa wapo salama."

Siwatu alikuwa amekaa kwenye kigoda, sasa akakaa chini ya mkeka, machozi yakaanza kumtoka, na baadaye akaangua kilio kwa sauti.

Ikabidi aanze kumbembeleza, lakini hakubembelezeka.

"Bakari, kwa muda wa miezi mitatu nimeishi na wewe, pamoja na kwamba tumetengwa, lakini sijawahi kuishi kwa amani na furaha kama tulivyokuwa wote hapa. Na ndiyo maana sikujali kutengwa kote huku. Leo unaondoka, nitaishi vipi mimi..." Akasema na kuendelea kulia kwa kwikwi.

Wakati huo walikuwa subuleni, kwani nyumbani aliyoachiwa na wazazi wake ilikuwa ni ya vyomba viwili na sebule.

"Unasikia Siwatu, usilie. Mimi pia sijawahi kuishi maisha ya furaha kama niliyoishi hapa, pamoja na changamoto za hapa na pale. Sitosahau wema wako wote ulionitendea. Wewe ndiye uliyenifanya niendelee kuishi. Mimi nakwenda nyumbani. Najua safari ni hatua, najua nitaondoka na utakavyosikia na mimi nitakavyosikia mpweke. Nimezoea kutembelea na wewe kwenda shamba, kurudi, kuokota kuni wote, kuchota maji, kula pamoja, nitamisi upendo wako, kwa maana hiyo sitokusahau kamwe. Hakuhakikishia nakwenda nyumbani, lakini nitarejea tena hapa." Yalikuwa ni maneno ya Bakari ambayo hata yeye mwenyewe alipokuwa akiongea, alijikuta machozi yakianza kumtiririka bila hata mwenyewe kujua.

"Si kweli, si kweli Bakari, unanisahau. Ukienda kwenu, ukikaa tu baada ya wiki mbili tatu na kuzoea tena mazingira ya kwetu, hutoweza kukumbuka huku kijijini kwa jinsi ulivyoishi kwa kutengwa." Bado Siwatu alikuwa akilia.

Jinsi alivyokuwa akiishi na Bakari, hakuona kama anaweza kuishi tena na mtu mwingine kama vile. Ni miezi mitatu ambayo aliiona kama anaishi peponi.

"Hapana, kwa sababu niienda huko, nitaeleza jinsi nilivyoepuka kifo, na nitawaeleza ndugu na familia yangu mtu ambaye ameniokoa. Sidhani kama kuna kukusahau hapo. Nyamaza. Ni uchungu kwa kweli. Hata mimi nina uchungu sana kuachana na wewe, ngoja tu kwanza niende, Mungu akipenda tutaonana."

Kwa upendo wa hali ya juu, wakajikuta wamekumbatiana. Wakakumbatia kwa muda mrefu huku kila mmoja akitamani kuendelea kuwa na mwenzake, lakini haiwezekani. Baadaye wakakumbuka kuwa wanaitana kaka na dada. Wakaachiana.

"Sasa unaondoka lini?" Akauliza Siwatu kwa sauti ya kichovu kama mtu ambaye ametoka kulia msiba wa wazazi wake wiki nzima.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# SINGIDA BIG STARS KUSAJILI WA DARAJA JUU

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Timu ya Singida Big Stars umeweka wazi kwamba, wanafanya usajili wa wachezaji wa daraja la juu ili kutofanya makosa ambayo yatawarudisha Championship.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Idara ya Habari wa Singida Big Stars, Hussein Massanza alisema kwa sasa Bodi ya Wakurugezi inapitia ripoti ya benchi la ufundi kwa ajili ya kuangalia nafasi za usajili wa wachezaji watakaoboresha kikosi chao.

Alisema malengo yao makubwa ni kufanya usajili mzuri wa wachezaji ambao watakaosaidia timu yao kufanya vizuri na kuleta ushindani mkubwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

"Kuhusu wachezaji wanaohusishwa na Singida Big Stars hizo ni taarifa, lakini kwa sasa bado hatujaanza mazungumzo na mchezaji yeyote kwa sababu bodi ipo katika mchakato wa kupitia ripoti ya tathmini ya Championship," alisema.

"Kuhusu mabadiliko ya benchi la ufundi bado liko miongoni mwa viongozi wa juu, kwa sababu tumejiandaa kufanya usajili mzuri na tishio ili kuleta ushindani katika ligi kuu."



Wachezaji wa timu ya taifa ya wasichana chini ya Umri wa miaka 17, Serengeti Girls, wakiwa kwenye mazoezi katika Uwanja wa Mao Zedong, Zanzibar, kujiandaa na mchezo wa marudiano kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Cameroon utakaochezwa Juni 5, 2022. **PICHA:TFF**

# Timu ya mieleka yajifua mashindano ya A. Mashariki

**Na Saada Akida**

TIMU ya taifa ya mchezo wa mieleka inaendelea na mazoezi ya kujiandaa na mashindano ya Afrika Mashariki yanayotarajiwa kufanyika Septemba Mwaka huu nchini Uganda.

Mashindano hayo yatashirikisha nchi saba ikiwamo Tanzania, Kenya, Rwanda, Burundi, Sudan, DRC Congo na Uganda ambao ni wenyeji wa michuano hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Shirikisho la Mieleka ya Ridhaa Tanzania, (TAWF) Andrew Kapelela, alisema kikosi cha wachezaji nane wanaendelea na kambi kwa ajili ya kujiweka vizuri na mchezo huo.

Alisema hatua ya sasa wanatekeleza kufanikisha masuala ya utawala ikiwamo kuhakikisha timu inakwenda katika mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka.

"Maandalizi yanaendelea vizuri na sasa tupo katika mchakato wa kufanikisha masuala ya utawala ilituweze kujua namna ya ushiriki wetu kwa kuongeza idadi ya wachezaji," alisema Kapelela.

Alisema wanaandaa timu hiyo kwa ajili ya kwenda kushindana na kupeperusha vema bendera ya Taifa ili mwaka mwingine kupata uwenyeji wa mashindano hayo.

"Mwaka huu tuliomba kuwa wenyeji, lakini ilishindika kwa sababu ni wachanga na shirikisho letu lina muda mfupi tangu limepata usajili hali ambayo inatufanya kukosa uwenyeji wa michuano hiyo," alisema.

Alisema mwaka huu timu hiyo ikienda kufanya vizuri huko wana matumaini makubwa ya mwaka mwingine kupewa uwenyeji.

## Rapa Kibonge atoa onyo wezi wa kazi zake

**Na Sabato Kasika**

RAPA wa kike, Kibonge Mwepec ameonya wale wanaotumia jasho lake kujinufaisha kuacha mara moja na kuwakumbusha kuwa jasho la mtu haliliwi.

Akizungumza na gazeti hili jana, msanii huyo alisema kuna watu wameweka nyimbo zake kwenye mtandao wa kuuzia kazi na hivyo kuwafanya wafaidike.

"Ninawakumbusha kuwa jasho la mtu haliliwi, waondoe nyimbo zangu mara moja," alisema Kibonge.

Alizitaja baadhi ya nyimbo hizo kuwa ni 'Jirani, Sharifa na Buku Jero' ambazo amedai kuwa kuna watu wameziingiza kwenye mitandao na blogs.

"Yaani nikirajibu kuingiza nyimbo zangu, inaonekana tayari zimeshaingizwa. Huu ni uhuni, watu wajue kuwa jasho la mtu haliliwi," alisema.

Alisema hayuko tayari kuona uhuni huo ukiendelea, na kwamba kila mtu ale kulingana na urefu wa kamba yake, siyo kuishia kiujanja ujanja.

"Muziki umeingiliwa na wahuni, nami siko tayari kuvumilia uhuni wa aina yoyote kwenye kazi zangu, siwezi kukubali hujuma hizi ziendelee," alisema.

## Tanzania kupeleka wa5 michuano ya tenis

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya dunia ya mchezo wa tenis yanatarajiwa kutimua vumbi Julai Mosi mwaka huu nchini Rwanda ambayo yamegawanyika makundi manne.

Mwenyekiti wa Chama cha Tenis Tanzania, (TTA) Denis Makoi, ameliambia gazeti hili kuwa watapeleka timu yenye wachezaji watano.

Alisema maandalizi kuelekea katika mashindano hayo yanaendelea vizuri na kwamba wiki ijayo wanatarajia kupeleka barua Baraza la Michezo Tanzani (BMT) kwa lengo la kuiomba serikali iwasaidie fedha ambazo zitasaidia safari nzima ya wachezaji hao.

"Tunaendelea na maandalizi tukishirikiana na Shirikisho la Mchezo wa Tenis Duniani (ITF) kuhakikisha tunakwenda kushiriki michuano hiyo," alisema Makoi.

Alisema ni mashindano ambayo yatakuwa magumu kwani kwa upande wa Tanzania ni mara ya kwanza kushiriki michuano hiyo mikubwa.

"Lengo letu ni kufanya vizuri na kurudi na medali ya ushindi nyumbani ikiwa pamoja na kuipeperusha vema bendera yetu. Nawaomba wadau pamoja na taasisi mbalimbali kujitokeza kuiunga mkono timu hii ili ifanye vizuri katika michuano hiyo."

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LACAZETTE KURUDI LYON
KLABU ya Lyon inataka kumnunua tena mshambuliaji wa Ufaransa, Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 31, kwa uhamisho huru - miaka mitano baada ya kumuuza kwenda Arsenal kwa pauni milioni 46.5. (***L'Equipe***)

### TIELEMANS HUYO ARSENAL
ARSENAL pia inataka kumsajili kiungo wa kati wa Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25, ambaye ataondoka Leicester City msimu huu wa joto. (***Fabrizio Romano, Twitter***)

### ASENSIO AWINDWA
KLABU ya Manchester United itapewa fursa ya kumsajili winga wa Real Madrid, Marco Asensio mwenye umri wa miaka 26. (***El Chiringuito***)

### LUKAKU NA BARCA
BARCELONA wanatarajiwa kuelekeza mawazo yao kwa mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 29, ikiwa hawataweza kumsajili Robert Lewandowski, mshambuliaji wa Poland mwenye umri wa miaka 33 ambaye anatazamiwa kuondoka Bayern Munich. (***Mundo Deportivo***)

### JESUS KUONDOKA
MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 25 na mlinzi wa Ukraine, Oleksandr Zinchenko mwenye miaka 25, wote wanaweza kuondoka msimu huu wa joto, huku winga wa England, Raheem Sterling mwenye miaka 27, anaweza kwenda timu nyingine ya daraja la juu. (***The athletic***)

### JESUS AWINDWA
ARSENAL wamemfanya Gabriel Jesus kuwa chaguo lao namba moja ingawa wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Juventus katika mbio za kumnunua mchezaji huyo wa zamani wa Palmeiras. (***Mirror***)

### AKE KUONDOKA
MLINZI wa Uholanzi, Nathan Ake mwenye umri wa miaka 27, pia ameambiwa anaweza kuondoka Manchester City na hilo linaweza kufungua njia ya kuhamia Newcastle. (***Talksports***)

### BOTMAN AGOMBEWA
MLINZI wa Uholanzi, Sven Botman mwenye umri wa miaka 22 anataka kuondoka Lille msimu huu wa joto na amesema AC Milan na Newcastle wana nia ya kumsajili. (***Algemeen Dagblad, via Chronicle***)

### SOUCEK HUYO SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur imepewa nafasi ya kumsajili kiungo wa kati wa West Ham kutoka Jamhuri ya Czech, Tomas Soucek, huku mazungumzo kuhusu mkataba mpya kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 yakiwa yamekwama. (***Football Insider***)

### JESSE ANYATIWA
AS Roma inamnyatia kiungo wa kati wa England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 29, mkataba wake na Manchester United utakapokamilika msimu huu, lakini West Ham na Everton miongoni mwa wanaomsarandia kiungo huyo. (***Gazzetta dello Sport***)

### KRISTENSEN NA LEEDS
KLABU ya Leeds United ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili beki wa kulia wa Red Bull Salzburg na Denmark, Rasmus Kristensen mwenye umri wa miaka 24. (***Sky Sports***).

### MEE ANAONDOKA
KLABU ya Burnley iliyoshuka daraja inatarajia nahodha wake, Ben Mee mwenye umri wa miaka 32 kuondoka msimu huu wa joto, na hivyo kuacha pengo kubwa katika kundi la wachezaji viongozi huku nahodha msaidizi na mlinzi mwenzake, James Tarkowski mwenye miaka 29, pia akitarajiwa kuondoka. (***Usajili unahitajika***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DE BRUYNE: NASUBIRI KWA HAMU KUCHEZA NA HAALAND

**Asema uwepo wa nyota huyo utamsaidia yeye kuendelea kuwa kwenye kiwango bora cha asisti na...**

**BRUSSELS,** UBELGIJI

KEVIN De Bruyne amesema ama subiri kwa hamu kubwa kucheza pamoja na "mshambuliaji wa kiwango cha juu" Erling Haaland pale Manchester City, akikiri kuwasili kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 kunaweza kumwezesha kuendeleza kwenye asisti zake ambazo tayari ni za kuvutia.

De Bruyne alichaguliwa kuwa Mchezaji Bora wa Ligi Kuu ya England wakati City ikishinda taji lao la nne la ligi ndani ya misimu mitano mwezi uliopita, huku kiungo huyo akifunga mabao 15 kwa msimu wa 2021-2022.

Haaland alifunga mabao 86 katika mechi 89 alizoichezea Borussia Dortmund baada ya kujiunga nayo akitokea RB Salzburg Januari 2020, na anatarajiwa kuimarika zaidi huku De Bruyne akimsubiria kumpa asisti za kutosha pale kwenye dimba la Etihad.

> **Akizungumza na jarida la Ubelgiji la HLN, De Bruyne alisema kuwa usajili wa Haaland hapo ulikuwa habari njema kwa timu na yeye mwenyewe.**

"Erling Haaland ni mshambuliaji wa kiwango cha juu. Kiwango chake kinapaswa kutusaidia kukua kama timu," alisema.

"Kila mtu anatarajia mengi kutoka kwake. Klabu imekuwa ikitafuta namba tisa, lakini nadhani itakuwa vizuri kuwa na mshambuliaji huyo ambaye anafunga mabao 20 hadi 25 kwa msimu."

Alipoulizwa kama ujio wa raia huyo wa Norway utamsaidia kuongeza ubunifu, De Bruyne aliongeza: "Labda. Kumekuwa na miaka ambayo nina pasi nyingi za mabao.

"Lakini uundaaji wangu wa nafasi na mambo mengine yamebaki sawa. Namba ni sehemu ya soka, lakini hazikuelezei habari kamili."

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,001,6

MECHI KALI
ITALY
VERSUS
GERMANY
1 | 2.81
X | 3.24
2 | 2.47

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MARTINEZ ATAKA KUBAKI INTER MILAN




**BUENOS AIRES, Argentina**

LAURATO Martinez amesisitiza nia yake ya kutaka kubakia Inter Milan huku kukiwa na tetesi za uhamisho wa kwenda Chelsea, akisema "mpango wangu uko wazi".

Idara ya Utamaduni, Vyombo vya Habari na Michezo ilithibitisha Jumatatu kwamba Chelsea haipo tena chini ya vikwazo vya serikali ya England baada ya mauzo ya klabu hiyo kwa muungano unaoongozwa na Todd Boehly.

Wamiliki wapya wanatarajiwa kuwekeza fedha nyingi katika dirisha lijalo la usajili ili kuimarisha kikosi hicho cha kocha, Thomas Tuchel ili kuweza kushindana na Manchester City na Liverpool.

Martinez amekuwa akihusishwa mara kwa mara na kuhamia Chelsea, huku Tuchel akijaribu kumuunganisha tena na nyota wa zamani wa Inter, Romelu Lukaku baada ya wawili hao kuwatumikia Nerazzurri hao na kutwaa taji la Scudetto msimu uliopita.

Hata hivyo, Martinez ameweka wazi nia yake huku akieleza matumaini yake ya kubakia Inter.

"Mpango wangu uko wazi," aliwaambia waandishi wa habari. "Nataka sana kubaki Inter msimu ujao.

"Sijapata mawasiliano yoyote kutoka kwa klabu hadi leo, nataka kuendelea na Inter msimu ujao."

Inter tayari wamempoteza Ivan Perisic kwa kocha wa zamani Antonio Conte kule Tottenham Hotspur, wakati Alessandro Bastoni anaweza kumfuata Mkroatia huyo kaskazini mwa London.

Kikosi hicho cha kocha Simone Inzaghi kinatarajiwa kumleta mshambuliaji wa Juventus, Paulo Dybala mkataba wake utakapomalizika, na hivyo kumpa Martinez fursa ya kuungana na mchezaji mwenzake wa kimataifa wa Argentina.

Martinez alikuwa katika kiwango kizuri cha kufunga kwenye Serie A msimu huu, akifunga mabao 21 katika mechi 35 - ni Ciro Immobile (27) wa Lazio pekee na Dusan Vlahovic (34) waliofanikiwa kufunga mabao zaidi ya Ligi Kuu ya Italia.

Inzaghi atatumaini kubaki na mchezaji wake huyo msimu ujao huku wakilenga kunyakua taji lililonyakuliwa na wapinzani wao AC Milan katika msimu wa 2021-22.

# Tite: Neymar anang'aa zaidi Brazil kuliko PSG

**SEOUL, Korea Kusini**

KOCHA wa Brazil, Tite amesema Neymar ana ushawishi zaidi akiwa na kikosi cha timu ya taifa Korea kuliko Paris Saint-Germain, kwa sababu timu hiyo inamtumikia zaidi.

Neymar alikuwa katika hali nzuri Brazil ilipoilaza Korea Kusini 5-1 katika mechi ya kirafiki Alhamisi, huku nyota huyo wa PSG akifunga penalti mbili.

Pasi zake nane muhimu zilikuwa zaidi ya mara mbili ya idadi iliyorekodiwa na mtu mwingine yeyote uwanjani, kwani Korea Kusini ilishindwa kukabiliana naye.

Kiwango cha Neymar kwenye mchezo huo uliopigwa hapa Seoul kilikuwa bora zaidi kuliko alivyocheza akiwa na PSG msimu huu, huku mabingwa hao wa Ligue 1 wakionekana kuwa tayari kumwachia aondoke.

Na Tite ametoa maoni yake kwa nini Neymar anaonekana muhimu zaidi kwa Brazil.

"Neymar ni upinde na mshale, kulingana na mazingira ya mchezo," alisema Tite akiwaambia waandishi wa habari.

"Akiwa PSG, mara nyingi anacheza sehemu ndogo zaidi ya Lionel Messi na Kylian Mbappe. Sio hapa, yeye ni mshale zaidi.

"Timu inafanya kazi ya ziada kumchezesha. Tuna timu inayomuunga sana mkono."

Matokeo ya Alhamisi yalikuwa ya kuvutia, huku Brazil ikitengeneza nafasi nyingi dhidi ya wenyeji.

"Timu ya Brazil imekuwa katika kiwango (fulani) cha uchezaji katika michezo yetu ya hivi karibuni," alienndelea.

Brazil itabakia katika ukanda huu kwa mechi ya kirafiki ya Jumatatu dhidi ya Japan kule Tokyo.

641,108/-

# SURE BOY AKERWA NA WACHAMBUZI

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa Yanga, Aboubakar Salum 'Sure Boy', amewataka wachambuzi wa habari za michezo kutowakatisha tamaa wachezaji wanaotoka timu moja kwenda nyingine, badala yake wawape moyo ili wafanye bidii ya mazoezi na kujituma na kupata namba.

Kiungo huyo ambaye ni mtoto wa winga wa zamani wa klabu za Sigara ya Yanga, Salum Abobakar 'Sure Boy', alisema wakati anakwenda Yanga watu walisema mengi, hasa wachambuzi wa habari za michezo kuwa hawezi kwenda kupata namba kwenye kikosi hicho kwa sababu kimesheheni wachezaji wengi wazuri kutoka nje kwenye nafasi anayocheza.

"Kwanza hili jambo nataka nilizungumze leo nimepata nafasi nashukuru Mungu, acha niliseme. Watu walizungumza sana hasa wachambuzi wengi, nilikuwa sipendi na ilikuwa wananikera, ila nilikuwa sitaki kuzungumza kwa sababu mimi ni mchezaji inabidi nionyeshe kwa miguu na si maneno," alisema Sure Boy.

"Mchezaji wakati anatoka sehemu moja hadi nyingine ni lazima atakuta watu, ni lazima atakutana na changamoto. Mimi wakati natoka Azam nilikuwa nimejipanga nikijua kwa nini naenda Yanga, kwa nini anaenda kufanya, nilikuwa nawaona kina Aucho (Klalid), Bangala (Yannick), ni wachezaji wakubwa wa nje, kweli wazuri, lakini nilijua naenda na nitapata nafasi kwa sababu najiamini na najua nini naenda kufanya."

Alisema yeye katika maisha yake hajawahi kukata tamaa na ndiyo siri kubwa ya kutowasilikiza waliokuwa wakizungumza.

"Mimi katika maisha yangu sijawahi kukata tamaa, hata nilipotoka changamoto nyingi nilikutana nazo, na mchezaji ili ukue ni lazima ukutane na changamoto, watu wanakuja kwenye timu na kuondoka wanaondoka, huwezi kuwa wewe tu peke yako kwenye namba unayocheza," aliongeza.

Mchezaji huyo alisajiliwa katikati ya msimu huu kipindi cha dirisha dogo na sasa amekuwa ni gumzo kwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo.



Msanii wa muziki wa kizazi kimpya, Ben Pol ambaye ni balozi wa Justdinggt akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuwatambulisha mabalozi wapya pamoja na uzinduzi wa wimbo mpya wa kuhamasisha utunzaji wa mazingira Tanzania. Kushoto ni Christina Shusho na Joh Makini. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Nahodha Coastal aikamia Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

NAHODHA wa Klabu ya Coastal Union, Pascal Kitenge, amesema amejipanga vizuri akishirikiana na wenzake kufanya vizuri katika mchezo wao dhidi ya Yanga utakaopigwa Juni 15 mwaka.

Akizungumza na gazeti hili, Pascal alisema lengo lao ni kupata pointi tatu katika mchezo huo.

"Tunaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kukutana na timu ya Yanga kwenye mchezo wetu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na tumejipanga vizuri sana kuhakikisha tunaibuka na ushindi," alisema Pascal.

Nahodha huyo alisema mchezo huo unatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa kwani watakutana na timu ambayo haijapoteza mchezo wowote wa ligi hadi sasa.

Alisema watafuata mbinu pamoja na maelekezo wanayoendelea kupewa na Kocha wao Mkuu, Juma Mgunda kuelekea kwenye mchezo huo.

Alisema anawashukuru mashabiki wao kwa ushirikiano wanaoaonyesha kipindi hiki cha Ligi Kuu licha ya kutokufanya vizuri kwenye michezo ya nyuma iliyopita.


## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/06/22 | 18:00 | Atletico Tucuman vs Colon de Santa Fe | 2.90 | 3.15 | 2.42 |
| 02. 04/06/22 | 19:00 | Finland vs Bosnia & Herzegovina | 2.60 | 3.05 | 2.70 |
| 03. 04/06/22 | 19:00 | Lithuania vs Luxembourg | 3.20 | 3.00 | 2.30 |
| 04. 04/06/22 | 21:45 | Montenegro vs Romania | 2.95 | 3.05 | 2.43 |
| 05. 04/06/22 | 21:45 | Italy vs Germany | 2.48 | 3.25 | 2.70 |
| 06. 05/06/22 | 01:00 | CA Patronato Parana vs Velez Sarsfield | 3.05 | 3.10 | 2.32 |
| 07. 05/06/22 | 01:00 | CA Platense vs CD Godoy Cruz | 2.95 | 3.25 | 2.31 |
| 08. 05/06/22 | 02:00 | Vancouver Whitecaps FC vs Real Salt Lake | 2.43 | 3.30 | 2.75 |
| 09. 05/06/22 | 02:30 | AC Goianiense GO vs SC Corinthians SP | 2.95 | 3.00 | 2.46 |
| 10. 05/06/22 | 08:00 | Renofa Yamaguchi vs Thespakusatsu | 2.55 | 3.05 | 2.80 |
| 11. 05/06/22 | 08:00 | Omiya Ardija vs Mito Hollyhock | 2.70 | 3.30 | 2.44 |
| 12. 05/06/22 | 08:00 | JEF United Ichihara Chiba vs Vegalta Sendai | 2.46 | 3.05 | 2.90 |
| 13. 05/06/22 | 08:00 | Blaublitz Akita vs Roasso Kumamoto | 2.85 | 3.00 | 2.50 |
| 14. 05/06/22 | 17:00 | EC Juventude RS vs Fluminense FC RJ | 2.80 | 3.00 | 2.60 |
| 15. 05/06/22 | 19:00 | Union de Santa Fe vs CA Tigre | 2.30 | 3.00 | 3.20 |
| 16. 05/06/22 | 21:45 | Kosovo vs Greece | 3.05 | 3.25 | 2.25 |
| 17. 05/06/22 | 22:00 | SE Palmeiras SP vs Atletico Mineiro MG | 2.28 | 3.20 | 3.05 |

## MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 04/06/2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 4550 | Saudi Arabia Youth vs Panama Youth | 5.30 | 3.63 | 1.57 |
| 15:00 | 4833 | Follo vs Sprint/Jeloy | 1.64 | 4.53 | 3.69 |
| 15:00 | 5348 | Staal Jorpeland vs Ullern | 2.35 | 3.78 | 2.44 |
| 15:00 | 5385 | Oppsal IF vs Os TF | 2.15 | 3.62 | 2.79 |
| 15:00 | 5841 | Brodd vs Bremnes | 1.99 | 4.24 | 2.76 |
| 16:00 | 1084 | Iraq U23 vs Australia U23 | 3.70 | 3.01 | 2.01 |
| 16:00 | 1161 | Paide Linnameeskond vs Viljandi Tulevik | 1.15 | 7.80 | 12.00 |
| 16:00 | 2201 | Lysekloster vs Sola | 1.76 | 3.95 | 3.85 |
| 16:00 | 2525 | Armenia vs Ireland | 4.14 | 3.38 | 1.88 |
| 16:00 | 4722 | Besiktas JK U19 vs Galatasaray U19 | 2.71 | 3.40 | 2.29 |
| 16:00 | 4811 | Turkmenistan U23 vs Iran U23 | 11.80 | 5.31 | 1.21 |
| 16:00 | 4997 | Gottne IF vs Storfors Aik | 1.36 | 4.81 | 6.28 |
| 16:00 | 5006 | FK Haugesund 2 vs Fana | 10.77 | 7.05 | 1.16 |
| 16:00 | 5152 | Atiker Konyaspor U19 vs Kayserispor U19 | 1.76 | 3.60 | 3.95 |
| 16:00 | 5268 | Caykur Rizespor U19 vs Kasimpasa U19 | 2.61 | 3.25 | 2.44 |
| 16:00 | 5785 | Denmark U21 vs Kazakhstan U21 | 1.08 | 7.82 | 23.47 |
| 16:00 | 5793 | Steinkjer vs Byaasen Toppfotball | 9.85 | 6.89 | 1.17 |
| 17:00 | 1167 | Qviding Fif vs Vanersborgs IF | 2.25 | 3.49 | 2.71 |
| 17:00 | 1206 | Aatvidaberg vs Falkenbergs | 3.33 | 3.38 | 1.99 |
| 17:00 | 1369 | Fylkir vs IF Vestri | 1.57 | 4.32 | 4.32 |
| 17:00 | 1422 | Randesund IL vs Pors Grenland | 6.11 | 5.12 | 1.35 |
| 17:00 | 1474 | DalvikÂk/Reynir vs Sindri | 1.96 | 4.11 | 2.89 |
| 17:00 | 2368 | Eslovs BK vs FK Karlskrona | 2.85 | 3.20 | 2.29 |
| 17:00 | 2508 | FC Chiasso vs Etoile Carouge FC | 1.77 | 3.63 | 3.87 |
| 17:00 | 2668 | Bergnasets Aik vs IF Algarna | 2.70 | 4.22 | 2.03 |
| 17:00 | 2842 | IK Gauthiod vs Saffle FF | 1.57 | 4.13 | 4.52 |
| 17:00 | 4543 | Skjetten vs Lillestrom SK 2 | 2.99 | 4.12 | 1.91 |
| 17:00 | 5588 | Oskarshamns Aik vs Ljungskille | 2.19 | 3.50 | 2.81 |
| 17:00 | 5645 | Vanersborgs FK vs Grebbestads IF | 2.44 | 3.87 | 2.31 |
| 17:00 | 5866 | Motala Aif vs Taby FK | 1.95 | 3.67 | 3.18 |
| 17:00 | 5893 | Sandviks IK vs Bodens BK | 6.49 | 4.92 | 1.35 |
| 17:30 | 3419 | Chertanovo Moskva W vs FC Lokomotiv Moscow W | 10.76 | 5.68 | 1.20 |
| 18:00 | 1652 | Ryazan Vdv W vs CSKA Moscow W | 8.83 | 4.32 | 1.32 |
| 18:00 | 2848 | Qatar U23 vs Uzbekistan U23 | 3.53 | 2.99 | 2.08 |
| 18:30 | 1026 | Fjardabyggd vs Njarovik | 7.60 | 6.00 | 1.28 |
| 18:30 | 1717 | France U18 vs Argentina Youth | 1.86 | 3.24 | 3.92 |
| 19:00 | 1383 | GD Fontinhas vs USC Paredes | 2.06 | 2.99 | 3.58 |
| 19:00 | 2619 | Legionovia vs Unia Skierniewice | 1.36 | 4.81 | 6.28 |
| 19:00 | 4179 | Lithuania vs Luxembourg | 3.23 | 3.03 | 2.32 |
| 19:00 | 4896 | Finland vs Bosnia and Herzegovina | 2.63 | 3.09 | 2.73 |
| 19:00 | 5207 | FC Rotenberg vs SC Bregenz | 1.95 | 3.43 | 3.38 |
| 19:00 | 5306 | Andorra U21 vs Kosovo U21 | 4.82 | 3.94 | 1.57 |
| 19:00 | 5970 | Hungary vs England | 8.09 | 4.14 | 1.42 |
| 20:00 | 1397 | Switzerland U21 vs Bulgaria U21 | 1.32 | 4.72 | 7.68 |
| 20:00 | 4378 | Kuwait U23 vs Jordan U23 | 3.38 | 2.99 | 2.13 |
| 21:45 | 1795 | Montenegro vs Romania | 2.97 | 3.07 | 2.45 |
| 21:45 | 3136 | Turkey vs Faroe Islands | 1.12 | 7.67 | 21.20 |
| 21:45 | 4555 | Italy vs Germany | 2.81 | 3.24 | 2.47 |
| 22:00 | 5620 | Las Palmas UD vs Tenerife | 1.90 | 3.24 | 4.09 |
| 22:30 | 5762 | America Mineiro MG vs Cuiaba MT | 1.79 | 3.19 | 4.42 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumamosi Juni 4, 2022
Nipashe



## De Bruyne: Nasubiri kwa hamu kucheza na Haaland



Wachezaji wa Timu ya Taifa, Taifa Stars, wakiwa kwenye mazoezi pamoja na kocha msaidizi, Shadrack Nsajigwa, wakijiandaa kuivaa Niger leo kwenye mchezo wa kufuzu michuano ya mataifa ya Afrika, AFCON. **PICHA:TFF**

# TAIFA STARS YAANZA KUISAKA AFCON LEO

## ●●●Inaivaa Niger nchini Benin baada ya viwanja vyake vya nyumbani kufungiwa kwa kutokuwa na vigezo na...

**Na Adam Fungamwango**

LEO saa moja usiku kwa saa za Afrika Mashariki, timu ya taifa ya soka ya Tanzania, Taifa Stars itatupa karata yake ya kwanza kwenye kinyang'anyiro cha kusaka tiketi ya kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) nchini Ivory Coast mwakani, itakapopambana na Timu ya Taifa ya Niger.

Mchezo huo utapigwa kwenye uwanja wa L'amitie jijini Cotonou nchini Benin.

Niger haichezi nchini kwao kutokana na viwanja vya huko kutokidhi vigezo vya Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Nahodha ya timu hiyo, Mbwana Samatta amesema timu imejiandaa vizuri kupata ushindi ili kujiweka kwenye mazingira mazuri na morali ya kuendelea kufanya vizuri kwenye kundi lake.

"Tunataka kuanza vizuri, na kwa bahati mbaya tunaanzia ugenini, lakini bahati nzuri pia ni kwamba iwapo tutashinda ugenini itakuwa imetupa morali kubwa ya kuendelea kufanya vizuri kwenye mechi zinazofuata," alisema Samatta.

Aliongeza; "najua itakuwa mechi ngumu kwa sababu hata Niger nao wanatamani kushiriki fainali za AFCON mwakani, sisi pia tunataka kushiriki miaka mitatu iliyopita, kila timu inaamini ikianza vizuri itakuwa kwenye nafasi nzuri, ila sisi tuna imani kuwa tutapata matokeo tunayoyataka.

"Zamani ilikuwa ngumu sana kwetu kushinda ugenini, lakini kwenye kutafuta nafasi ya kufuzu Kombe la Dunia tulishinda mechi ugenini, kwa hiyo imetupa kujiamini kuwa tunaweza kushinda popote hata kwenye michuano hii," alisema Samatta anayeichezea Royal Antwep FC ya Ubelgiji kwa mkopo kutokea Fenerbahce ya Uturuki.

Stars itakuwa inacheza kwenye uwanja iliouzoea kwani Oktoba 10, mwaka jana, ilicheza dhidi ya wenyeji Benin na kushinda bao 1-0 lililofungwa na Simom Msuva kwenye michuano ya kusaka tiketi ya kufuzu Kombe la Dunia litakalofanyika mwishoni mwa mwaka huu nchini Qatar.

Stars ipo kwenye Kundi F, pamoja na timu za Niger, Algeria, na Uganda.

Fainali za AFCON zinatarajiwa kuchezwa nchini Ivory Coast Juni 23, na Julai 23 mwakani.

## Barbara: Simba tunamleta kocha wa kiwango cha juu

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba ikiwa katika mchakato wa kutafuta kocha mpya kukinoa kikosi cha timu hiyo, Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara Gonzalez amesema hawafanyi mambo ya kubahatisha katika usajili na kuleta watu wenye daraja kubwa kwa ajili ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba kwa sasa wako katika mchakato wa kupitia majina na CV za makocha hao huku Mohammed Adil Errad akitajwa kuwa na asilimia kubwa ya kuchukuwa nafasi ya Pablo Franco aliyeondolewa hivi karibuni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Barbara alisema kwa sasa wako katika mchakato mzuri wa kutafuta kocha pamoja na usajili wao ikiwamo kuboresha kikosi cha timu yao kwa kuleta wachezaji ambao watasaidia Simba kufikia malengo yao ya kucheza nusu fainali ya Afrika.

Alisema wanafanya usajili kulingana na mahitaji ya benchi la ufundi na kuboresha sehemu nyeti na hawafanyi usajili kwa ajili ya sifa au kukomoa klabu fulani.

"Simba hatufanyi mambo kwa kubahatisha na kupiga kelele kama wengine, sisi tunasajili wachezaji wa daraja la juu ambao wataifanya timu iwe imara zaidi," alisema.

Aliongeza kusema kuwa sababu kamati ya usajili ina weledi na uzoefu mkubwa wa usajili ana matarajio makubwa kikosi cha msimu ujao kitakuwa bora na imara kwa ajili ya kufikia malengo yao ya kutimiza kiu ya kucheza nusu fainali.

Alisema hawatarudia makosa yaliyojitokeza msimu huu kwa sababu wanahitaji kufikia malengo yao hasa katika michuano ya kimataifa, na ni lazima wafanye usajili mkubwa na wachezaji wenye kiwango kikubwa na daraja la juu.

Simba wakiendelea kuficha jina la kocha huyo gazeti hili limepata taarifa kwamba Kocho Mohammed aliyewahi kufundisha APR anatarajiwa kuchukuwa mikoba ya Pablo na kutua nchini Tanzania mapema kushuhudia kikosi hicho kinapomalizia mechi zao za ligi ili kupata nafasi ya kushiriki katika usajili wa msimu ujao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >